LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
LHRC
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

# MUHTASARI WA RIPOTI YA HAKI ZA BINADAMU 2019

TANZANIA BARA

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*

**Kimetayarishwa na:**

Mr. Fundikila Wazambi na Ms. Joyce Komanya

**Kimehaririwa na:**
Bi. Anna Henga (Wakili)
Bi. Felista Mauya
Bw. Fulgence Massawe (Wakili)
Bi. Naemy Sillayo (Wakili)
Bw. Paul Mikongoti

**Kimechapishwa na:**
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu
Aprili, 2020

Kijitabu hiki hakiuzwi

Namba ya Kijitabu (ISBN): 987-9987-740-53-6

# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| Kuhusu Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu | ii |
| Utangulizi | ii |
| Sura ya Kwanza: Kuhusu Tanzania | 1 |
| Sura ya Pili: Haki za Kiraia na Kisiasa | 5 |
| Sura ya Tatu : Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni | 20 |
| Sura ya Nne : Haki za Kiujumla | 29 |
| Sura ya Tano : Haki za Makundi Maalum | 31 |
| Sura ya Sita: Mifumo ya Ulinzi wa Haki za Binadamu | 41 |
| Sura ya Saba: Hitimisho na Mapendekezo Muhimu | 46 |
| Mambo ya Jumla Yanayoathiri Ulinzi na Utekelezaji wa Haki za Binadamu | 42 |

## KUHUSU KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ni shirika binafsi, huru, la hiari, lisilo la kiserikali, lisilofungamana na chama chochote cha kisiasa na lisilotengeneza faida kwa ajili ya kugawana, ambalo linalenga kufikia jamii yenye haki na usawa. LHRC ina lengo la kuwawezesha Watanzania kukuza, kuimarisha na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini. Lengo kubwa la LHRC ni kujenga ufahamu wa sheria na haki za binadamu miongoni mwa umma na hasa watu walio kwenye hatari kubwa ya kunyimwa haki zao za msingi, kutoa elimu ya sheria na uraia, kufanya utetezi unaohusisha pia msaada wa kisheria, utafiti na ufuatiliaji wa haki za binadamu. LHRC ilianzishwa mwaka 1995 na inafanya kazi Tanzania Bara.

## UTANGULIZI

**Mambo na Matukio Makuu Yaliyogusa Ulinzi na Utekelezaji wa Haki za Binadamu kwa mwaka 2019**

***Mambo na Matukio Yaliyolenga Kuimarisha Ulinzi na Utekelezaji wa Haki za Binadamu***

Kutungwa na kutekelezwa kwa sheria ya makubaliano ya kukiri kosa katika mfumo wa utoaji haki kwa makosa ya jinai

Utafiti kuhusu rushwa ya ngono utakaofanywa na TAKUKURU

Kuteuliwa kwa Mwenyikiti wa Tume ya Haki za Binadamu na makamishna wa haki za binadamu

Uzinduaji wa mahakama zinazotembea na Mfumo wa TEHAMA wa kusajili na kuratibu Mashauri (JDS – 2)

Marekebisho ya Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015 kulinda haki ya kujieleza kupitia ufanyaji tafiti na utoaji takwimu

Maamuzi ya Mahakama ya Rufaa ya Tanzania yakikubaliana na hukumu ya Mahakama Kuu kwamba vifungu vinavyoruhusu ndoa za utotoni katika Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 vinakinzana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na hivyo vifanyiwe marekebisho ili kuweka umri wa miaka 18 kama umri wa kuoa na kuolewa

Serikali kuongeza juhudi za kuendeleza miundombinu, ikiwemo barabara, reli na madaraja

Hukumu ya Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki juu ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016

Uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura wakati Tanzania ikielekea kwenye chaguzi za Serikali za Mitaa 2019 na Uchaguzi Mkuu wa Rais na Wabunge 2020

Maamumuzi ya Mahakama ya Afrika ya Hazi za Watu na za Binadamu kuhusu adhabu ya kifo

Uletaji wa Kanuni za Kuongeza Kasi ya Usikilizaji wa Mashauri yanayoyahusu makundi maalum, ikiwemo wanawake, watu wenye ulemavu na watoto
Kuzinduliwa kwa mabaraza ya kuboresha stadi/sifa za ajira kwa wahitimu wa vyuo
Urasimishaji wa lugha ya alama

## Mambo na Matukio Yaliyoathiri Ulinzi na Utekelezaji wa Haki za Binadamu

Marekebisho ya Sheria ya Asasi zisizo za Kiserikali
Marekebisho ya Sheria ya Chama cha Wanasheria Tangayika
Tatizo la afya ya akili na kuongezeka kwa matukio ya watu kujiua
Mrundikano magerezani sababu ya idadi kubwa ya mahabusu
Tanzania kujitoa katika tamko linaloruhusu watu binafasi na asasi za kiraia kupeleka kesi katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Watu na Binadamu
Matukio ya ukatili dhidi ya Watoto kuwa mengi na kuongezeka, hasa ubakaji na ulawaiti
Matukio ya mimba za utotoni kuwa mengi na kuongezeka
Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na vyama vya siasa kujitoa katika uchaguzi huo
Matukio ya mauaji ya madereva bodaboda yanayofanywa na watu wasiojulikana
Kuongezeka kwa matukio ya wanawake wanaouliwa sababu ya wivu wa kimapenzi (ukatili wa kimwili dhidi ya wanawake)
Mauaji ya kikatili ya watoto mkoani Njombe

### Haki 5 zilizokiukwa zaidi mwaka 2019

| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|
| **Haki ya Kuishi** | **Uhuru dhidi ya Ukatili** | **Uhuru wa Kujieleza** | **Haki ya Kuwa Huru na Salama** | **Uhuru wa kukusanyika na Kujumuika** |
| Mauaji ya watoto, mauaji ya wanawake, mauaji yanayotokana na kujichukulia sheria mkononi, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina | Ukatili wa kingono na kimwili dhidi ya watoto; ukatili wa kingono na kimwili dhidi ya wanawake, ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu & wazee | Sheria kand-amizi, ukamataji na uwekaji kizuizini waadhishi wa habari kinyume na sheria, kufungiwa vyombo vya habari | Ukamataji na uwekaji watu kizuizini kinyume na sheria, kukataa kutoa dhamana, mauaji, utekaji | Kuminywa uhuru wa kukusanyika, sheria na kanuni kand-amizi |

## Madhumuni ya Ripoti na Ukusanyaji Taarifa

### Madhumuni

**Elimu ya haki za binadamu** – haki fulani inamaanisha na kujumuisha nini? Haki hiyo inalindwa na mfumo upi wa kisheria? Kwa nini haki hii ni muhimu? Haki hii ina mipaka ipi?

**Kukumbushia** – ni maeneo gani ya haki za binadamu yanahitaji kuimarishwa?

**Uchechemuzi wenye ushahidi** – nini kinahitaji kubadilika na kwa nini?

**Mambo na matukio yaliyosaidia ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu** – ni mambo au matukio gani yameimarisha ulinzi au utekelezaji wa haki za binadamu?

**Mambo na matukio yaliyoathiri ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu** – ni mambo au matukio gani yameathiri ulinzi na utekelezaji wa haki za binadamu?

**Uchambuzi wa sheria na miswada** – ni nini kimebdilika kufuatia utungwaji wa sheria au marekebisho ya sheria au kanuni? Mabadiliko hayo yameleta au yataleta athari gani kwenye haki za binadamu?

**Mapendekezo** – nini kifanyike kuimarisha na kulinda haki za binadamu?

**Utoaji taarifa** – kukutaarifu kuhusu haki za binadamu na masuala ya kisheria ili kuchukua tahadhari na kutekeleza wajibu wako kwa mujibu wa sheria mbalimbali za nchi.

**Kuonyesha mienendo** – hali ilikuwajie miaka ya nyuma ukilinganisha na sasa?

**Kutoa mwanga katika kupanga afua** – ripoti inaweza kutumika kama sehemu ya kuanzia katika kupanga afua mbalimbali.

**Kuelimisha** – kutoa elimu kuhusu haki za binadamu; elimu kuhusu mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu ya kitaifa, kikanda na kimataifa; elimu kuhusu masuala ya kisheria; elimu kuhusu mambo mapya kuhusu sheria na haki za binadamu.

### Ukusanyaji Taarifa

Taarifa zilizotumika kuandaa ripoti hii zimepatikana kutoka vyanzo mbalimbali, ikiwemo taarifa zilizopatikana kupitika shughuli za LHRC na huduma zinazotolewa kwa wanufaika, pamoja na mfumo wa LHRC wa kufuatilia haki za binadamu. Vyanzo vingine vya uhakika ni pamoja na ripoti na matamko mbalimbali ya Serikali na wadau wasio wa kiserikali na utafiti kuhusu haki za binadamu na biashara uliofanywa na LHRC mwaka 2019. Pia, utafiti wa LHRC wa taarifa zilizotolewa na vyombo vya habari kwa mwaka 2019 ulitoa taarifa muhimu zilizosaidia uandaaji wa ripoti hii ya haki za binadamu, ikiwemo kuwezesha ufanyaji wa utafiti zaidi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na sheria na haki za binadamu

**Muundo wa Ripoti**

| | |
|---|---|
| **Sura ya 1: Kuhusu Tanzania** | Inaelezea kwa kifupi kuhusu Tanzania, ikigusia historia, jiografia, idadi ya watu na mihimili ya serikali, na wajibu wa mihimili hii katika ulinzi wa haki za binadamu |
| **Sura ya 2: Haki za Kiraia na Kisiasa** | Inaelezea hali ya haki za msingi za kiraia na kisiasa, ikiwemo uhuru wa kujumuika na kukusanyika; uhuru wa kujieleza; haki ya usawa mbele ya sheria na kupata nafuu ya kisheria; haki ya kuishi |
| **Sura ya 3: Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni** | Inaelezea haki muhimu za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, ikiwemo haki ya kufanya kazi, haki ya elimu, haki ya afya na haki ya maji safi na salama |
| **Sura ya 4: Haki za Kiujumla** | Inaangazia hali ya haki za kiujumla, hususan haki ya maendeleo na haki ya kufurahia na kufaidika na rasilimali asilia. |
| **Sura ya 5: Haki za Makundi Maalum** | Inaelezea hali ya haki za wanawake, watoto, watu wenye ulemavu, wazee na watu wanaoishi na VVU |
| **Sura ya 6: Mifumo ya Ulinzi wa Haki za Binadamu** | Inaangazia mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu katika ngazi za kitaifa, kikanda, na kimataifa na kujadili wajibu wake katika ulinzi wa haki za binadamu. |
| **Sura ya 7: Hitimisho na Mapendekezo** | Inatoa hitimisho kuhusu haki za binadamu na kutoa mapendekezo yayatakayosaidia kukusa na kuimarisha ulinzi wa haki za biandamu nchini Tanzania. |

# SURA YA KWANZA: KUHUSU TANZANIA

## 1.1. Historia

Kabla ya kutawaliwa na wakoloni wa Kijerumani na Kiingereza katika Karne ya 19, Tanganyika (sasa Tanzania Bara) ilikaliwa na wazawa waliokuwa wakizungumza lugha ya Kibantu, ambao baadae walipata ugeni toka Bara la Asia na toka Uarabuni. Kufikia Karne ya 15 Wareno nao wakaingia; na katika kipindi hicho cha Waarabu na Wareno, ndipo biashara ya utumwa ilipamba moto. Ilipofika mwaka 1880 ulifanyika mkutano mkubwa katika Mji wa Berlin – Ujerumani, ambapo nchi za Ulaya zililigawa Bara la Afrika kwa ajili ya kulitawala. Ujerumani ilipewa sehemu mbalimbali za Afrika Mashariki, ikiwemo Tanganyika. Baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, Tanganyika iliwekwa chini ya ukoloni wa Uingereza, mpaka ilipofikia mwaka 1961, ambapo Tanganyika ilipata uhuru. Katika kipindi chote cha ukoloni, machifu mbalimbali walipigana na uongozi kandamizi wa kikoloni, **ambao ulikandamiza haki zao kama binadamu**, akiwemo Mtemi Mirambo wa Wanyamwezi, Mangi Meli wa Wachagga na Abushri wa Pangani. Mapigano makubwa zaidi yalitokea Mwaka 1905 wakati wa ukoloni wa Mjerumani, yakifahamika zaidi kama Vita vya Majimaji, ambavyo viliongozwa na kiongozi wa kimila na kiroho aliyeitwa Kinjekitile Ngwale, ambaye aliaminika kuwa na uwezo wa kugeuza risasi kuwa maji.

Harakati za kupata uhuru ziliongozwa na chama cha TANU (Tanganyika African National Union), ambacho kilizaliwa mwaka 1954, kabla ya hapo kikifahamika kama TAA (Tanganyika African Association), kilichoanzishwa mwaka 1929. Kiongozi wa chama alikuwa Mwl. Julius Nyerere, ambaye aliiongoza TANU na Tanganyika kupata uhuru mwaka 1961, akiwa Waziri Mkuu wa Kwanza chini ya **Katiba ya Uhuru**. Mwaka 1962, Tanganyika ikawa Jamhuri, Nyerere akiwa Rais wake wa kwanza chini ya **Katiba ya Jamhuri**, ambayo ilimfanya kuwa Kiongozi wa Taifa, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu, pia akiwa sehemu ya Bunge. Mwaka 1964, Tanganyika iliungana na Zanzibar, ambayo ilikuwa imepata uhuru toka kwa Sultani wa Oman mwaka 1963, na kuunda Tanzania. Katiba ya tatu, **Katiba ya Muungano**, iliundwa, ikileta mfumo wa serikali mbili, chini ya vyama vya TANU (Tanzania Bara) na ASP (Zanzibar). Mwaka 1965, **Katiba ya Mpito** iliundwa, ambayo ilirudisha nchi katika mfumo wa chama kimoja. Katiba hii ilipitishwa kama sheria nyingine za bunge, kinyume na kanuni za kikatiba. Mwaka 1977, vyama vya siasa vya TANU na ASP viliungana na kuunda Chama cha Mapinduzi (CCM), ambacho kilitengeneza **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977**, ambayo ndio inayotumika mpaka leo, japo imekuwa ikifanyiwa marekebisho mbalimbali yapatayo kumi na nne mpaka mwaka 2015. Mojawapo ya marekebisho makubwa ni yale ya mwaka 1992, ambayo yalirudisha **mfumo wa vyama vingi**. Mengine ni yale ya mwaka 1984, ambayo hatimaye yaliingiza **hati ya haki za binadamu kwenye Katiba.** Kabla ya hapo, tangu nchi ipate uhuru, haki za binadamu hazikuonekana kuwa muhimu sana kuwekwa kwenye Katiba, japo Tanzania ilikuwa imeshaanza kuridhia baadhi ya mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu.

## 1.2. Jiografia

Tanzania iko kati ya Latitudo 10 na 120 Kusini na Longitudo 290 na 410 Mashariki. Inapakana na Bahari ya Hindi upande wa Mashariki na imepakana na nchi za Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi na Zambia kwa pande nyingine. Tanzania ndio nchi kubwa kuliko zote Afrika Mashariki na kuna Mlima Kilimanjaro, ambao ndio mlima mrefu kuliko yote barani Afrika, wa tatu duniani. Tanzania imebarikiwa kuwa na maliasili nyingi, ikiwemo mimea, mabonde ya ufa, maziwa, mito na mbuga za wanyama. Maziwa ni pamoja na Ziwa Victoria - ambalo ni kubwa kuliko yote Afrika, na Ziwa Tanganyika - ambalo lina kina kirefu kuliko yote Afrika. Mbuga za wanyama ni pamoja na Serengeti, Mikumi, Manyara, Ngorongoro na Katavi.

## 1.3. Idadi ya Watu

Idadi ya watu Tanzania inaendelea kuongezeka, ambapo kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, idadi ya watu ni 43,625,354 kwa Tanzania Bara na 1,303,569 kwa Zanzibar. Wanawake ni wengi zaidi (51.3%) ukilinganisha na wanaume (48.7%). Kufikia mwaka 2016, idadi ya watu iliongezeka hadi kufikia takribani 50,144,175, huku 24,412,889 wakiwa wanaume na 25,731,286 wakiwa wanawake. Idadi kubwa ya watu wapo vijijini kuliko mijini.

## 1.4. Mihimili ya dola na wajibu wa mihili hiyo katika ulinzi wa haki za binadamu

Kuna mihimili mikuu mitatu ya dola nchini Tanzania, ambayo ni: Serikali, Bunge na Mahakama. Mihimili hii imeanzishwa na kupewa mamlaka na **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.**

### A. Serikali Kuu

Serikali inajumuisha Rais - ambaye ni Kiongozi wa Taifa, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu - na Baraza la Mawaziri. Baraza la mawaziri linajumuisha Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Rais wa Zanzibar na mawaziri wote. Rais ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri. Makamu wa Rais anamsaidia Rais kwenye mambo yote ya muungano. Zanzibar ina serikali yake na Rais wake chini ya mfumo wa serikali mbili ambao Tanzania unautumia, na ina mamlaka juu mambo yote ambayo sio ya muungano, kama yalivyoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wajibu katika ulinzi wa haki za binadamu: Wajibu wa Serikali Kuu ni pamoja na kutekeleza majukumu yake chini ya mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia; kuilinda Katiba, ambayo inajumuisha haki za binadamu; kuhakikisha utekelezaji wa haki za Kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kwa kutoa huduma za kijamii kama vile maji, afya na elimu; kulinda haki ya kuwa huru na salama kupitia vyombo vya dola na mifumo ya haki; kutuoa ulinzi wa kisheria na ki-haki za binadamu kupitia Jeshi la Polisi, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na wizara husika katika sekta mbalimbali.

**Marais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

**Mw. Julius Kambarage Nyerere: 1964-1985**
**Ali Hassan Mwinyi: 1985-1995**
**Benjamin William Mkapa: 1995-2005**
**Jakaya Mrisho Kikwete: 2005-2015**
**John Pombe Magufuli: 2015- mpaka sasa**

## B. Bunge

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio chombo kikuu cha kutengeneza sheria nchini, ambacho kinaundwa na wabunge mbalimbali wa chama tawala (CCM) na vyama vya upinzani. Rais pia ni sehemu ya Bunge kwa mujibu wa Katiba. Kazi kuu ya bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali. Bunge hili lina mamlaka juu ya mambo yote ya muungano. Zanzibar ina Baraza la Wawakilishi, ambacho ndio chombo chake kikuu cha kutengeneza sheria na kuisimamia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Bunge lina wabunge wa kuchaguliwa na wabunge wa kuteuliwa.

Wajibu katika ulinzi wa haki za binadamu: Utungaji wa sheria za kulinda haki za binadamu; uridhiaji wa mikataba na utungwaji wa sheria za kusaidia utekelezaji wa mikataba hiyo; kuisimamia na kuishauri Serikali katika utekelezaji wa shughuli zake; kujadili masuala mbalimbali yanayohusiana na haki za binadamu na kuyatolea maamuzi.

## C. Mhimili wa Mahakama

Mahakama ni chombo kikuu cha utoaji haki nchiniTanzania, ambapo kuna mahakama kadhaa ambazo zinatofautiana kimamlaka. Mahakama ya juu kabisa ni Mahakama ya Rufaa, ambayo ina majaji wa Mahakama ya Rufaa, ambao husimamia na kutolea maamuzi kesi zote za rufaa. Ya pili ni Mahakama Kuu, ambayo pia ina majaji (Majaji wa Mahakama Kuu), ambao husimamia kesi zote katika ngazi hiyo na kuzitolea maamuzi. Mahakama zinazofuatia ni Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo – ambayo ndio mahakama ya chini kabisa. Tofauti na Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu, mahakama hizi za chini zina mahakimu. Mahakama Kuu ina vitengo mbalimbali, ikiwemo cha ardhi, biashara, kazi na cha rushwa – ambacho kiliundwa mwaka 2016. Majaji wanateuliwa na Rais baada ya kupata ushauri wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, huku mahakimu wakichaguliwa na Tume hiyo moja kwa moja. Pia kuna **Mahakama Maalum ya Katiba,** ambayo ina mamlaka ya kushughulikia kesi za kikatiba, ikiwemo haki za binadamu. Ukiacha mahakama hizi, kuna mahakama za kijeshi-ambazo ni mahsusi kwa ajili ya wanajeshi.

Mahakama ya Rufaa ni mahakama yenye mamlaka hadi Zanzibar, ambayo pia ina mahakama zake ziitwazo Mahamaka Kuu ya Zanzibar, Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanzo. Pia kuna Mahakama ya Rufaa ya Kadhi na Mahakama ya Kadhi.

Wajibu katika ulinzi wa haki za binadamu: Mhimili huu una wajibu mkubwa katika ulinzi wa haki za binadamu, ikiwemo kutafsiri sheria mbalimbali, ikiwemo zinazohusu haki za binadamu; kuchukua hatua za kisheria dhidi ya watuhumiwa wa vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu; na kusikiliza madai yanayohusiana na haki za binadamu. Mhimili huu pia hufanya mapitio ya maamuzi na vitendo vya watu na mamlaka mbalimbali kulingana na viwango vya haki za binadamu; huimarisha upatikanaji wa haki; hukuza utaratibu wa kisheria; na hutengeneza sheria kupitia kesi.

# SURA YA PILI: HAKI ZA KIRAIA NA KISIASA

## Utangulizi

**Haki Zilizoangaliwa (9)**

Haki ya Kuishi, Uhuru wa Kujieleza, Haki za Usawa mbele ya Sheria na Nafuu ya Kisheria, Haki ya Kuwa Huru na Salama, Haki ya Kutoteswa, Uhuru wa Kukusanyika, Uhuru wa Kujumuika, Haki ya Kushiriki katika Utawala au Serikali

Haki za kiraia na kisiasa zinalindwa kwenye mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu. Mikataba hii ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR) wa mwaka 1966, Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (ACHPR), Mkataba wa Nyongeza katika Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu juu ya Haki za Wanawake barani Afrika (Maputo Protocol) na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC). Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pia inajumuisha haki za binadamu, zikiwemo haki za kiraia na kisiasa. Ripoti hii imejikita katika haki muhimu tisa, kama zilivyotajawa hapo juu**.**

## 2.1. Haki ya Kuishi

Haki ya Kuishi iliendelea kuathiriwa na matukio ya kujichukulia sheria mkononi, mauaji yanayotokana na maafisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi, ukatili dhidi ya maafisa wa vyombo vya dola, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, mashumbulizi dhidi ya watu wenye ualbino, adhabu za kifo, ajali za barabarani, mauaji ya kikatili ya watoto mkoani Njombe na mauaji ya wanawake yanayotokana na wivu wa kimapenzi.

### Maauaji yanayotokana na wananchi kujichukulia sheria mkononi

Japokuwa mienendo ya matukio ya mauaji yanayotokana na watu kujichukulia sheria mkononi yanaonekana kupungua katika miaka ya hivi karibuni, kuanzia mwaka 2015, idadi ya matukio hayo bado iko juu. Taarifa za Jeshi la Polisi za kufikia mwezi Juni 2018 zinaonyesha kwamba jumla ya matukio 385 ya mauaji yanayotokana na watu kujichukulia sheria mkononi yaliripotiwa katika kipindi hicho, sawa na wastani wa mauaji 76 kwa mwezi. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikusanya matukio 8 ya mauaji yanayotokana na watu kujichukulia sheria mkononi, ambayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Kagera, Shinyanga, Dar es Salaam, Ruvuma, Mtwara na Dodoma.

**Maoni ya LHRC:** Ni hatari na ni ukiukwaji wa haki za binadamu kwa watu kujichukulia sheria mkononi. Hii inaweza kuwa ni dalili ya watu kutokuwa na imani na mfumo wa haki; lakini pia inaweza kuwa kiashiria cha watu kuwa na uelewa mdogo kuhusu mfumo wa haki jinai, ikiwemo masuala ya dhamana zinazotolewa kisheria kwa makosa mbalimbali ya jinai, hivyo kupelekea

watuhumiwa wa makosa hayo kuonekana tena mtaani wakati uchunguzi au kesi vikiendelea polisi na mahakamani.

**Mauaji yanayotokana na maafisa wa vyombo vya dola kutumia nguvu kupita kiasi na ukatili unaonfanywa dhidi ya maafisa wa vyombo hivyo**

Kwa upande wa mauaji yanayotokana na maafisa wa vyombo vya dola kutumuia nguvu kupita kiasi kwa mwaka 2019, ni matukio matatu (3) ambayo LHRC iliweza kupata taarifa zake, ambayo ni matukio mawili (2) pungufu ya yale yaliyoripotiwa mwaka 2018. Matukio haya ya mwaka 2019 yaliripotiwa katika Mikoa ya Kilimanjaro, Geita na Pwani. Kwa upande mwingine, tukio moja (1) la ukatili dhidi ya maafisa wa vyombo vya dola liliripotiwa katika Wilaya ya Nyang'hwale mkoani Geita, ambapo maafisa polisi watatu (3) kutoka kituo cha polisi wilayani humo walijeruhiwa na watu wenye hasira baada ya kuingilia kati kumnusuru mtuhimwa wa ujambazi waliyekuwa wanampiga.

**Wito wa LHRC:** Maafisa polisi kuepuka utumiaji wa nguvu kupita kiasi pale wanapomkamata mtuhumiwa na kumweka chini ya ulinzi au mahabusu kama inavyoelekezwa na viwango mbalimbali vya kitaifa na kimataifa kuhusu ukamataji na uwekaji kizuizini wa watuhumiwa, ikiwemo Kanuni za Kudumu za Jeshi la Polisi na Kanuni za Umoja wa Mataifa za Utendaji Kazi wa Maafisa wa Vyombo vya Dola.

**Wito wa LHRC:** Wanajamii kuepuka kuwashambulia maafisa wa vyombo vya dola kwa sababu ni kosa kisheria na ni ukiukwaji wa haki zao kama binadamu. Vilevile, ni jambo la hatari kwa wanajamii kuwashambulia maafisa wa vyombo vya dola kwani sheria inawaruhusu kutumia nguvu kiasi kujilinda, ikiwemo matumizi ya silaha za moto, pale ambapo maisha yao hapo hatarini.

**Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino**

Katika miaka ya karibuni, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina yamekuwa yakipungua, sababu mojawapo ikiwa na hatua zinazochukuliwa na Jeshi la Polisi kupambana na uhalifu huu katika mikoa ambayo mauaji hayo hutokea zaidi, kama vile Tabora na Shinyanga. Takwimu za hivi karibuni za Jeshi la Polisi zinaonyesha kwamba katika kipindi cha mwezi Januari hadi Juni 2018, jumla ya matukio 106 ya mauaji ya aina hiyo yaliripotiwa katika vituo vya polisi. Kwa mwaka 2016, Kituo hakikufanikiwa kupata takwimu za polisi, lakini kiliweza kukusanya matukio 6 ya mauaji yanayotokana na imani za kishirikina yaliyoripotiwa katika Mikoa ya Mbeya, Dar es Salaam, Simiyu, Tabora na Shinyanga. Mauaji ya kikatili ya watoto mkoani


**Mashambulizi na mauaji dhidii ya watu wenye ualbino yanatokana na imani za kishirikina. Baadhi ya watu huamini kwamba viungo vya watu wenye ualbino vinaweza kutumika kutengeneza dawa ya kuwaletea bahati au kuwafanya wawe matajiri.**

Njombe, ambayo yalianza tangu mwishoni mwa mwaka 2018 na kuendelea hadi mwanzoni mwa 2019, yaliripotiwa pia kuhusishwa na imani za kishirikina.

Watu wenye ualbino waliendelea kuishi kwa hofu, hii ikisababishwa na mashambulizi dhidi yao yanayotokana na imani za kishirikina. Mienendo inaonyesha kwamba mashambuilizi dhidi ya watu wenye ualbino huongezeka katika kipindi cha uchaguzi, lakini kwa mwaka 2019, ambao ulikuwa mwaka wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ni matukio mawili tu ya mashambulizi dhidi ya watu wenye ualbino yaliripotiwa, ikiwemo tukio moja la kufukua kaburi la mtu mwenye ualbino. Hata hivyo, bado watu wenye ualbino wameendelea kuishi kwa hofu katika kipindi hichi ambacho Tanzania inaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

**Adhabu ya kifo**

Kwa mwaka 2019, idadi ya matukio ya adhabu ya kifo yaliyokusanywa na LHRC ni 19, ambayo ni matukio 14 pungufu ya yale yaliyoripotiwa mwaka 2018. Kwa sasa, kuna wafungwa zaidi ya 480 ambao wanasubiri kunyongwa, wengi wao (90%) wakiwa ni wanaume. Kuongezeka huku kwa idadi ya adhabu za kifo kunakuja katika kipindi ambacho Mahakama ya Afrika ya Haki za Watu na Binadamu imetoa hukumu dhidi ya adhabu ya kifo katika kesi ya **Ally Rajabu na wengine dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.** Katika hukumu iliyotolewa mwezi Novemba mwaka 2019, Mahakama hiyo yenye makao yake jijini Arusha nchini Tanzania iliilekeza nchi ya Tanzania kufanya marekebisho katika sheria yake ya makosa ya jinai (Kanuni za Adhabu) na kuondoa adhabu ya lazima ya kifo, kwani adhabu hiyo ya lazima inakiuka Mkataba wa Afrika wa Haki za Watu na Binadamu.





**Matukio ya adhabu za kifo yaliyokusanywa na LHRC mwaka 2017 hadi mwaka 2019**

**Wito wa LHRC:** Tanzania tayari ni nchi ambayo imeshaacha kutekeleza adhabu ya kifo na hivyo haina budi kupiga hatua mbele zaidi na kusaini na kuridhia Mkataba wa Pili wa Nyongeza

wa Mkataba wa Haki za Kiraia na Kisiasa, ambao umelenga kuondoa Adhabu ya Kifo wa Mwaka 1991. Pia, nchi nyingi duniani zimeondoa adhabu ya kifo katika sheria zake na hivyo basi Tanzania pia inaweza kufanya hivyo. Mpaka kufikia mwezi Disemba mwaka 2017, jumla ya nchi 106 duniani zilikuwa zimeondoa adhabu ya kifo, ikiwemo nchi jirani za Msumbiji na Rwanda. Katika miaka ya karibuni, nchi za Bara la Afrika ambazo zimeondoa adhabu ya kifo katika sheria zake ni pamoja na Madagascar (2015), Benini (2016), Guinea (2017) and Burkina Faso (2018). Kwa sasa, ni nchi takribani 53 tu duniani zimeendelea kuwa na adhabu ya kifo kwenye sheria zake na kutekeleza adhabu hiyo; na katika nchi hizo, nchi 29, ikiwemo Tanzania, zimeendelea kuwa nchi ambazo zinatoa adhabu ya kifo lakini hazitekelezi adhabu hiyo.

Ajali za barabarani

Kwa mwaka 2019, ajali za barabarani na vifo vinavyotokana na ajali hizo viliendelea kupungua. Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Juni 2019, jumla ya ajali 1,610 zilitokea na kusabababisha vifo 781. Katika kipindi hicho hicho kwa mwaka 2018, jumla ya ajali 2,220 za barabarani zilitokea na kusababisha vifo 1,051. Hata hivyo, pamoja na kupungua kwa ajali na vifo, bado idadi ya matukio ni kubwa, ikiwa ni wastani wa ajali 268 na vifo 130 kila mwezi kwa mwaka 2019. Ajali nyingi za barabarani zinagusa haki za binadamu kwa sababu zinatokana na uendeshaji kasi, ulevi, matumizi ya madawa ya kulevya, kutovaa kofia ngumu kwa upande wa pikipiki, pamoja na kutovaa mkanda kwa upande wa magari.




**Matukio ya ajali za barabarani yaliyoripotiwa vituo vya polisi pamoja na vifo vilivyotokana na ajali hizo – mwezi Januari hadi mwezi Juni mwaka 2018 & 2019**

## Mauaji ya kikatili ya watoto mkoani Njombe

Haki ya watoto ya kuishi ilihatarishwa na kukiukwa kufuatia mauaji ya kikatili ya watoto mkoani Njombe, ambayo yalianza mwishoni mwa mwaka 2018 hadi mwanzoni mwa mwaka 2019. Baadhi ya miili ya watoto hao ilikutwa ikiwa haina baadhi ya viungo vya mwili, ikiwemo sehemu za siri. Miongoni mwa watoto waliouawa ni pamoja na watoto 3 wa familia moja. Mauaji hayo yalihusishwa na imani za kishirikina

Mauaji ya wanawake yanayotokana na wivu wa kimapenzi

Mwaka 2019 ulishuhudia kuongezeka kwa mauaji ya wanawake yanayotokana na wivu wa kimapenzi. Ripoti ya hivi karibuni ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti Madawa ya Kulevya na Uhalifu inaonyesha kwamba nyumbani imekuwa sehemu hatari zaidi kwa wanawake kufuatia matukio ya ukatili na mauaji ya wanawake.

## 2.2. Uhuru wa Kujieleza

Kwa ujumla, uhuru wa kujieleza ulidorora kiasi mwaka 2019, kwa sababu mbalimbali, ikiwemo: utekelezaji wa sheria zinazominya uhuru huo; adhabu kali kwa vyombo vya habari, ikiwemo kufungiwa; na ukamataji na uwekaji kuzuizini wa waandishi wa habari kinyume na sheria.

Sheria kandamizi na hukumu ya Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki dhidi ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016

Sheria kandamizi ziliendelea kuwa kikwazo katika utekelezaji na ufurahiaji wa uhuru wa kujieleza nchini Tanzania. Mwezi Machi 2019, Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki ilitoa hukumu yake kuhusu Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016, kufuatia kesi iliyofunguliwa na LHRC, Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC). Katika hukumu hiyo, Mahakama ilithibitisha vifungu vya 7(3) (a), (b), (c), (f), (g), (h), (i) na (j); vifungu vya 19,20 na 21; vifungu vya 35,36,37,38,39 na 40; vifungu vya 50 na 54; vifungu vya 52 na 53; na vifungu vya 58 na 59 kuwa vinakiuka haki ya uhuru wa kujieleza na Mkataba unaoanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Marekebisho ya Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015 kuboresha uhuru wa kujieleza.

Mwaka 2019 ulishuhudia marekebisho chanya ya Sheria ya Takwimu ya mwaka 2015 baada ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitisha marekebisho ya sheria hiyo kwa kuondoa na kurekebisha vifungu ambavyo vilikuwa ni vikwazo katika kufurahia na kutekeleza uhuru wa kujieleza, ikiwemo kukataza uchapishaji wa takwimu bila ya ridhaa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu na kuchapisha takwimu ambazo zinakinzana na takwimu rasmi.

Ukamataji na/au uwekaji kizuizini wa waandishi wa habari kinyume na sheria

Matukio ya ukamataji wa waandishi wa habari kinyume na sheria kwa mwaka 2019 ni pamoja na tukio la ukamataji wa Erick Kabendera na Joseph Gandye. Kwa mujimu wa THRDC, katika kipindi cha mwezi Januari hadi Septemba 2019, matukio 13 zaidi ya ukamati wa waandishi wa habari kinyume na sheria yaliripotiwa.

Adhabu za kufungiwa na kulipa faini kwa vyombo vya habari: Mwaka 2019, LHRC ilikusanya matukio manne ya vyombo vya habari kupewa adhabu ya kufungiwa na kulipa faini kwa madai ya kukiuka Kanuni za Maudhui ya Mtandao, ambazo zimekuwa zikilalamikiwa kutoendana na viwango vya kimataifa vya uhuru wa kujieleza. Vyombo hivyo vya habari ni Gazeti la The Citizen, na televisheni za mtandaoni za Kwanza Online TV, Watetezi TV na Ayo TV.

**Sheria nyingine zinazoendelea kuminya uhuru wa kujieleza**
Ukiacha Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016, sheria nyingine ambazo ziliendelea kuminya uhuru wa kujieleza kupitia baadhi ya vifungu vyake ni pamoja na Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015, Sheria ya Upatikanaji Habari ya mwaka 2016, na Kanuni za Maudhui ya Mtandao. Sheria hizi zinajumuisha vifungu ambavyo havikidhi viwango vya kimataifa vya uhuru wa kujieleza. Uwepo na utekelezaji wa sheria hizi uliendelea kuchangia upunguaji wa nafasi ya ushiriki wa wananchi kwa mwaka 2019.

**Tanzania katika Viwango vya Uhuru wa Habari Duniani mwaka 2019**
Kwa mwaka 2019, Tanzania ilishuka kwa nafasi 25 katika viwango vya uhuru wa habari duniani, kutoka nafasi ya 93 kwa mwaka 2018 hadi nafasi ya 118 kwa mwaka 2019. Uwepo na utekelezaji wa sheria zinazominya uhuru wa kujieleza, kama zilivyoainishwa hapo juu, kumechangia kushuka katika viwango hivyo.

**Wito wa LHRC:** Serikali na Bunge kufanya juhudi na kuchukua hatua madhubuti kufanyia marekebisho sheria na kanuni zote zinazochangia kupungua kwa nafasi ya ushiriki nchini Tanzania ili sheria na kanuni hizo ziendane na viwango vya kimataifa vya uhuru wa kujieleza. Uhuru wa kujeleza, uhuru wa kukusanyika na uhuru wa kujumuika ni muhimu katika kupata maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Uwepo wa taasisi na asasi za kiraia ambazo ziko huru ni jambo zuri katika kipindi hichi ambacho Tanzania inaelekea kuwa nchi ya uchumi wa kati kupitia viwanda na maendeleo ya miundombinu.

### 2.3. Haki za Usawa mbele ya Sheria na Nafuu ya Kisheria

Haki ya usawa mbele ya sheria inajumuisha: upatikanaji wa haki, haki ya kuchukuliwa kama mtu asiye na hatia, haki ya uwakilishi wa kisheria na haki ya kesi/mashauri kuendeshwa kwa haki. Haki ya nafuu madhubuti ya kisheria ni haki ya msingi inayohusiana na haki ya usawa mbele ya sheria. Katika kipindi cha mwaka 2019, Serikali na Mhimili wa Mahakama ziliendelea kuchukua hatua mbalimbali kuboresha upatikanaji na ufikiaji wa haki. Hatua hizo ni pamoja na: ujenzi wa majengo ya mahakama na ukarabati wa majengo ya zamani; matumizi ya TEHAMA kuongeza kasi ya kushughulikia mashauri mahakamani na kupunguza gharama za kuhudhuria kesi; kuleta na kuanza kutoa huduma ya mahakama za kutembea; kutunga kanuni za kuwezesha mashauri au kesi zinazowahusu watu walio katika makundi maalum (wanawake, watu wenye ulemavu na watoto) kushughulikiwa kwa uharaka; ukaguzi wa mahakama; kutengeneza Mpango Kazi wa Pili wa Kitaifa wa Haki za Binadamu wa kipindi cha mwaka 2019 hadi mwaka 2023; uanzishwaji wa vituo jumuishi vya kutoa huduma za kimahakama; kufanyia mapitio mfumo wa haki jinai; kupunguza mrundikano wa kesi; na kutengeneza Mwongozo wa Utoaji Adhabu

Hatua zilizochukuliwa kuboresha upatikanaji na ufikiaji wa haki, kama zilivyotajwa hapo juu, zinaweza kuimarisha haki za binadamu nchini Tanzania na LHRC itaendelea kufuatilia utekelezaji wa hatua hizo ili kuona ni kwa kiasi gani zimechangia kuimarisha ufurahiaji na utekelezaji wa haki za usawa mbele ya sheria na nafuu madhubuti ya kisheria. Pamoja na hatua chanya zilizochukuliwa, kwa mwaka 2019 changamoto mbalimbali ziliendelea kuathiri ufurahiaji wa haki za usawa mbele ya sheria na nafuu madhubuti ya kisheria. Changamoto hizo ni pamoja na: makamanda wa Jeshi la Polisi kuwaonyesha watuhumiwa mbele ya vyombo vya habari; ucheleweshaji na uahirishaji wa mara kwa mara wa kesi katika mfumo wa haki jinai; changamoto ya upatikanaji na ufikiaji wa msaada wa kisheria kwa watu wanaoishi maeneo ya kijijini; mrundikano wa wafungwa na mahabusu magerezani; upungufu wa watumishi katika Mhimili wa Mahakama; na rushwa katika mfumo wa haki.


**Makamanda wa Jeshi la Polisi kuwaonyesha watuhumiwa mbele ya vyombo vya habari**

Suala ya kuwaonyesha watuhumiwa mbele ya vyombo vya habari liliibuka kama suala la msingi mwaka 2019. Mkuu wa Jeshi la Polisi, Ispekta Jenerali wa Polisi Simon Sirro, alikemea tabia hii wakati wa kikao kazi na Maafisa Waandamizi wa Jeshi la Polisi na Makamanda wa polisi Mkoa, ambapo aliwaonya Makamanda wa Polisi Mkoa dhidi ya tabia ya kuwaonyesha watuhumiwa mbele ya vyombo vya habari. Inspekta Jenerali wa Polisi alisema kwamba kufanya hivyo kunakiuka kanuni ya kutendewa kama mtu asiye na hatia ya kosa la jinai mpaka mahakama itakapothibitisha vinginevyo. Aliwakumbusha makamanda hao wa polisi kwamba wanatakiwa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kuwataka kutoingilia majukumu ya Mhimili wa Mahakama. Kuwaonyesha watuhumiwa wa makosa ya jinai mbele ya vyombo vya habari kunakiuka haki zao kama watuhuhumiwa na kanuni ya kutendewa kama mtu asiye na hatia ya kosa la jinali mpaka mahakama itakapothibitisha vyinginevyo. Tabia hii imepigwa marufuku katika nchi mbalimbali duniani, ikiwemo nchini Philippines katika miaka ya hivi karibuni. LHRC inapenda kumpongeza Inspekta Jenerali wa Polisi kwa kukemea tabia hii kwani Ibara ya 13(6)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inasemwa wazi kwamba "ni marufuku kwa mtu aliyeshitakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitka kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo."

**Haki ya kupata msaada wa kisheria kwa watu wanaoishi maeneo ya vijijini**

Suala la upatikanaji wa msaada wa kisheria, hususan kwa watu wanaoishi vijijini, lilionekana kuwa changamoto kwa mwaka 2019. Pamoja na juhudi za wadau wa kiserikali na wasio wa kiserikali kutoa msaada wa kisheria katika maeneo mbalimbali nchini Tanzania, bado uhitaji umekuwa ni mkubwa na kumekuwa na wasiwasi kwamba huduma za msaada wa kisheria zimejikita zaidi katika maeneo ya miji midogo na mijini.

## Mrundikano wa mahabusu na wafungwa magerezani




Suala la mrundikano wa mahabusu na wafungwa magerezani lilionekana kuwa tatizo kubwa mwaka 2019, ambapo iliripotiwa kwamba asilimia 54 ya watu walio magerezani kwa sasa ni mahabusu. Wakati alipotembelea Gereza la Butimba jijini Mwanza mwaka 2019, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Rais John Magufuli, alitoa amri kwa mamalaka husika, ukiwemo Mhimili wa Mahakama, kuchukua hatua Madhubuti kutatua tatizo la msongamano magerezani.

## Kutungwa kwa sheria ya makubaliano ya kukiri kosa

Mnamo Mwezi Septemba mwaka 2019, sheria ya makubaliano ya kukiri kosa ilipitishwa nchini Tanzania kupitia marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai (Sura ya 20). Marekebisho ya sheria hiyo yalipelekea kuletwa kwa makubaliano ya kukiri kosa – ambayo ni makubaliano kati ya mwendesha mashtaka na mtuhumiwa. Kuletwa kwa makubaliano haya kumepokelewa kwa hisia tofauti, ambapo kwa upande mmoja kumekuwa na wasiwasi kuhusu uwezekano wa ukiukwaji wa taratibu za kijinai na haki za mtuhumiwa, na kwa upande mwingine kuwa na haja ya kuongeza kasi ya upatikanaji haki. Kwa maoni ya LHRC, hatua ya kwanza katika kuweka mzani sawa ni kuhakikisha kwamba Mhimili wa Mahakama unakuwa sehemu ya makubaliano hayo, kama ilivyo katika nchi ya Singapore barani Asia.

*Faida za utaratibu wa makubaliano ya kukiri kosa*

- Mtuhumiwa/mshitakiwa anaweza kupewa adhabu ndogo zaidi.
- Mshitakiwa haitaji kucheza pata potea pale ambapo kesi itakapoanza kusikilizwa, ambapo maamuzi ya mahakama yanaweza yasiwe mazuri kwake na kesi inaweza kuchukua muda mrefu, kulingana na uzito wa kosa aliloshitaiwa.
- Makubaliano yanaweza kuokoa muda wa mshitakiwa, mwendesha mashtaka na mahakama.
- Mtuhumiwa anaweza kuokoa fedha nyingi ambazo angetumia kumlipa wakili wake.
- Makubaliano yatasaidia kupunguza mrundikano wa kesi mahakamani, hivyo kupunguza mzigo kwa waendesha mashtaka na mahakama (Mahakimu na Majaji) – kupelekea kupungua kwa ukubwa wa kazi na kuongeza 'ufanisi.'
- Kupunguza mrudikano wa mahabusu na wafungwa magerezani, kama makubaliano yatapelekea mtuhumiwa kuachiwa huru au kupewa adhabu ndogo zaidi.
- Mtuhumiwa kutoa taarifa muhimu kama sehemu ya makubaliano, ambazo zinasaidia kumkamata mtuhumiwa mkubwa zaidi au kupelekea kupatikana taarifa muhimu zaidi kuhusu kesi husika.

*Wasiwasi kuhusu makubaliano ya kukiri kosa*

- o Mtuhumiwa kushurutishwa na kutishiwa ili akiri kosa (kutokiri kosa kwa hiari)
- o Suala la mtuhumiwa kutokuwa na hatia kutopewa kipaumbele.
- o Ushauri mbaya kutoka kwa wakili au mwanasheria wa mshitakiwa.
- o Mwendesha mashtaka kuwa na nguvu ya kumtishia mtuhumiwa kwamba asipokubali makubaliano basi ataomba mahakama impatie adhabu ya juu zaidi, na pia uwezekano wa kutengenezwa mazingira ya rushwa ili mshtakiwa asipate adhabu kubwa.
- o Watu kuhamasika au kuhamasishwa kukiri makosa ambayo hawajafanya, huku mtu aliyefanya kosa akiendelea kufanya uhalifu katika jamii.
- o Kupunguzwa kwa mamlaka na nguvu ya Hakimu au Jaji, huku mwendesha mash taka akiwa na nguvu zaidi ya kuamua kesi.
- o Kuondoa uwezekano wa jina la mtuhumiwa wa kosa la jinai kusafishwa kwa kuwa amelazimika kukiri kosa ili aachiwe ama kupewa adhabu ndogo, bila kujali kama ni kweli alitenda kosa ama la.
- o Makubaliano kujikita zaidi kwa mtuhumiwa kuliko mhanga wa uhalifu.

**Ucheleweshaji na uahirishaji wa kesi katika mfumo wa haki jinai**

Pamoja na kupiga hatua kadhaa katika kuimarisha upatikanaji wa haki mwaka 2019, tatizo la ucheleweshaji na uahirishaji wa kesi liliendelea kuwa mwiba katika upatikanaji wa haki nchini Tanzania. Malalamiko kuhusu ucheleweshaji katika uchunguzi wa kesi unaofanywa na polisi pamoja na waendesha mashtaka kudai kwamba uchunguzi huajakamalika na kuomba kesi ipelekwe mbele yamekuwa ni mambo ya kawaida na yanayotokea mara kwa mara mahakamani. Ucheleweshaji na uahirishaji huu wa kesi unachangia mrundikano wa mahabausu na wafungwa katika magereza, hasa kwa kesi zinazohusisha makosa ambayo hayana dhamana.

**Upungufu wa watumishi wa mahakama, mahakimu na majaji**

Kwa mujimu wa Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, Mhimili wa Mahakama unakabiliwa na changamoto ya upungufu wa watumishi, ambapo kwa sasa kuna watumishi 5,947, huku idadi inayohitajika ikiwa ni 10,351, hivyo kuwepo kwa upungufu wa watumishi 4,404. Hii ni sawa na upungufu wa asilimia 42.5.

Mhimili wa Mahakama

42.5% Upungufu wa watumishi

**Rushwa ndani ya mfumo wa kimahakama**

Tatizo la rushwa limeendelea kuwa mwiba katika taasisi mbalimbli, ikiwemo mahakama. Kwa mwaka 2019, LHRC ilikusanya kesi mbili zinazowahusu mahakamu wawili ambao walishitakiwa na TAKUKURU mikoani Dar es Salaam na Shinyanga kwa kuomba na kupokea rushwa. Hizi ni kesi sita pungufu ya zile zilizoripotiwa mwaka 2018.

**Wito wa LHRC:** Wizara ya Katiba na Sheria kuongeza kasi ya uandaaji wa Mpango Kazi wa Pili wa Kitaifa wa Haki za Binadamu wa mwaka 2019 hadi mwaka 2023 na kukamilisha zoezi hilo, kwani tayari tuko mwaka 2020 na bado mpango kazi haujawa tayari.

## 2.4. Haki ya kuwa Huru na Salama

Kwa mwaka 2019, haki ya kuwa huru na salama ilihatarishwa ama kukiukwa kutokana na sababu mbalimbali, hususan mauaji ya madereva bodaboda; ukamataji na uwekaji kizuizini wa watuhumiwa kinyume na sheria, na matukio ya utekaji.

**Mashambulizi na mauaji ya madereva bodaboda**

Kwa mwaka 2019, matukio ya wizi wa pikipiki na mashambulizi dhidi ya madereva bodaboda yaliendelea kuwa changamoto katika ufurahiaji wa haku ya kuwa huru na salama kkwa upande wa madereva hao. Kwa mujibu wa takwimu za Jeshi la Polisi, katika kipindi cha mwezi Januari hadi mwezi Juni 2019, jumla ya matukio 2,329 ya wizi wa pikipiki yaliripotiwa, huku katika kipindi kama hicho mwaka 2018, jumla ya matukio ya wizi wa pikipiki 2,510 yaliripotiwa. Matukio haya ni mengi sana na yanahatarisha haki za kuishi na kuwa huru na salama za madereva bodaboda, kwani mara nyingine matukio haya huambatana na utekaji na mauaji ya madereva hao. Kwa mwaka 2019, LHRC ilikusanya jumla ya matukio manne (4) ya mauaji ya madereva bodaboda, ambao waliuawa baada ya kuporwa pikipiki zao kwa nguvu. Matukio hayo yaliripotiwa katika Mikoa ya Mbeya (3) na Shinyanga (1).

**Matukio ya utekaji, watu waliopotea na matukio ya ukamataji na uwekaji kizuizini kinyume na sheria**

Kwa mwaka 2019, tukio la utekaji wa mwanaharakati wa kisiasa, Bw. Mdude Nyagali, liliripotiwa mkoani Songwe. Mashuhuda wa tukio hilo walidai kwamba mtu huyo alichukuliwa kwa nguvu na watu wasiojulikana na akatoweka kwa siku nne kabla hajapatikana akiwa dhaifu na kama mtu aliyepigwa sana. Katika kipindi hichi pia, hakukuwa na taarifa mpya kuhusu kupotea kwa mwandishi wa habari Azory Gwanda, aliyepotea tangu mwaka 2017, na mwanasiasa Ben Saanane, aliyepotea mwaka 2016.

Katika kipindi cha mwaka 2019, LHRC ilikusanya matukio 17 ya ukamataji na uwekaji wa watu kizuizini kinyume na sheria, ikiwemo ukamataji na uwekaji kizuizini wa mfanyakazi wake, Bw. Tito Magoti. Idadi hii ya matukio inaonesha ongezeko la matukio yapatayo 8 ukilinganisha na matukio yaliyoripotiwa na kukusanywa na LHRC mwaka 2018. Kasoro kuu zilizojitokeza wakati wa ukamataji na uwekaji kuzuizini ni maafisa wakamataji kushindwa kujitambulisha kikamilifu, ikiwemo kuonyesha vitambulisho vyao; maafisa polisi kutowaeleza watuhumiwa sababu za kukamatwa kwao; kuwakatalia watuhumiwa haki ya uwakilishi na kuwahoji bila ya mawakili wao kuwepo; kukataa kutoa dhamana; na kushindwa kuwafikisha watuhumiwa mbele ya mahakama haraka iwezekanavyo (ndani ya masaa 24) kama inavyotakiwa kisheria

**Jumbe muhimu:**

- Mtuhumiwa ana haki ya kuambiwa sababu za kukamatwa kwake.
- Mtuhumiwa ana haki ya kuambiwa mapema iwezekanavyo mashtaka yanayomk abili.

- o Mtuhumiwa ana haki ya kumfikia na kupata usaidizi wa mwanasheria wake.
- o Mtuhumiwa ana haki ya kupelekwa mbele ya mahakama haraka iwezekanavyo (ndani ya masaa 24).
- o Mtuhumiwa ana haki ya kupewa dhamana wakati akisubiri kesi yake kusikilizwa, isipokuwa kwa makosa ambayo hayana dhamana.
- o Mtuhumiwa ana haki ya kuelezewa haki zake na afisa anayemkamata na namna ya kuweza kutekeleza haki hizo.
- o Mtuhumiwa ana haki ya kutendewa kama mtu asiye na hatia mpaka itakapothibit ishwa vinginevyo na mahakama.
- o Mtuhimiwa ana haki ya kutoa malalamiko kuhusu namna anavyotendewa na ma hakama na vyombo vya dola.
- o Mtuhumiwa ana haki ya shauri lake kusikilizwa kwa haki na kupata nafuu mad hubuti ya kisheria.
- o Haki inayocheleweshwa ni haki inayokataliwa.

**Haki ya kupata dhamana**

Haki ya kupata dhamana iliibuka kwenye mjadala mwaka 2019 baada ya Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma kupendekeza kwamba makosa yote kuwa na dhamana, pendekezo ambalo limeungwa mkono na wadau wengine mbalimbali. Kwa mujibu wa Jaji Mkuu, makosa yote yawe na dhamana, kama ilivyo kwa nchi jirani ya Kenya, huku Mhimili wa Mahakama ukiachwa kufanya maamuzi ya mwisho kuhusu utoaji wa dhamana.

**Uendeshaji wa mashtaka kabla ya uchunguzi kukamilika**

Kwa mwaka 2019, uendeshaji wa mashtaka kabla ya uchungzi kukamilika uliendelea kuwa changamoto inayoathiri haki ya kuwa huru na salama. Uendeshaji wa mashtaka kabla ya uchunguzi kukamilka huambatana na mtuhumiwa kuendelea kuteseka mahabusu au gerezani na unakikua kanuni ya kutendewa kama mtu asiye na hatia mpaka pale itakapothibitishwa vinginevyo na mahakama, kanuni ambayo ipo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na mikataba ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu ambayo Tanzania imeridhia.

**Wasiwasi na malalamiko kuhusu ubambikaji wa kesi**

Kwa mwaka 2019, suala la ubambikaji wa kesi kwa watu wasio na hatia lilielezewa na viongozi mbalimbali kama changamoto, ikiwemo Waziri wa Mambo ya Ndani, Mh. George Simbachawene.

## 2.5. Uhuru wa Kujumuika na Kukusanyika

Kwa mwaka 2019, uhuru wa kukusanyika na kujumuika uliendelea kuathiriwa na masuala mbalimbali, ikiwemo marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992, ambayo yalileta vifungu ambavyo vinakinzana na viwango vya kimataifa vya uhuru wa kujumuika na kukusanyika. Pia, mwaka 2019 kulitokea marekebisho ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, ambazo pia zililalamikiwa kukinzana na viwango vya kimataifa vya uhuru wa kujumuika.

### Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa

Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa yalikosolewa na wadau mbalimbali kwa kujumuisha vifungu ambavyo vinaminya uhuru wa kujumuika na kukusanyika kinyume na Katiba na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu. Mambo makuu ambayo yameonekana kuminya uhuru huu ni pamoja na: baadhi ya vifungu kutoeleweka vizuri, hivyo kuacha mianya ya watu wenye mamlaka kutumia vibaya madaraka yao kuminya haki hizo na kuleta hofu ya ufurahiaji wa haki hiyo; mamlaka makubwa aliyopewa Msajili wa Vyama vya Siasa, ambayo yanahatarisha kwa kiasi kikubwa uhuru wa vyama vya siasa; na adhabu kubwa kupita kiasi kwa makosa mbalimbali yaliyoanishwa katika sheria hiyo.

### Marekebisho ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika

Kama ilivyokuwa kwa marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, marekebisho ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika yalizua wasiwasi kuhusu haki ya uhuru wa kujumuika wa mashirika yasiyo ya kiserikali na Chama cha Wanasheria Tanganyika. Kwa upande wa marekebisho ya Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali vifungu ambavyo vimezuia wasiwasi ni pamoja na vile: vinavyotoa mamlaka makubwa kwa Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserkali, ikiwemo kuyafuta mashirika ambayo hayajajisajili upya kulingana na matakwa mapya ya kisheria; matakwa makubwa ya utoaji taarifa; na matakwa ya kujisajili upya baada ya muda uliotengwa na kupatiwa cheti kipya. Vifungu hivi vinakinzana viwango vya kikanda na kimataifa vya uhuru wa kujumuka na kukusanyika. Kwa upande wa Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika, changamoto kubwa zilizoletwa na marekebisho ya sheria hiyo ni kuingilia haki ya chama hicho kujipangia mambo yake na kufurahia uhuru wa kujumuika, pamoja na kuminya uhuru wa taasisi hiyo kama chama cha wanasheria.

### Malalamiko kuhusu uminyaji wa haki ya kukusanyika kinyume na sheria

Kwa mwaka 2019, kikwazo kikubwa katika ufurahiaji na utekelezaji wa uhuru wa kujumuika kwa upande wa vyama vya siasa ilikuwa na uminyaji wa uhuru wa kukusanyika, ambapo uhuru huo hautakiwi kutekelezwa na mwanasiasa nje ya jimbo lake. Vyama vya siasa, hususan vya upanzani, viliendelea kulalamikia maamuzi haya kwamba yanakiuka haki yao inayolindwa na Katiba, jambo linaloathiri pia ushindani wao kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Vyama hivi pia vililalamika kwamba marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa yanaminya uhuru wao wa kujumuika na kukusanyika.


**Malalamiko kuhusu uminyaji wa haki ya kukusanyika kinyume na sheria**
Kwa mwaka 2019, kikwazo kikubwa katika ufurahiaji na utekelezaji wa uhuru wa kujumuika kwa upande wa vyama vya siasa ilikuwa na uminyaji wa uhuru wa kukusanyika, ambapo uhuru huo hautakiwi kutekelezwa na mwanasiasa nje ya jimbo lake. Vyama vya siasa, hususan vya upanzani, viliendelea kulalamikia maamuzi haya kwamba yanakiuka haki yao inayolindwa na Katiba, jambo linaloathiri pia ushindani wao kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020. Vyama hivi pia vililalamika kwamba marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa yanaminya uhuru wao wa kujumuika na kukusanyika.

## 2.6. Haki ya Kushiriki katika Utawala au Serikali

**Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019**
Kwa mwaka 2019, jambo kuu lililohusisha haki ya kushiriki katika utawala au serikali lilikuwa ni haki ya kupiga na kugiwa kura kupitia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019. Uchaguzi huu ulifanyika mwezi wa Novemba 2019 na mambo makuu yaliyoibuka kufuatia uchaguzi huo ni pamoja na uandikishaji wa wapiga kura na watu waliojitokeza kupiga kura; elimu ya mpiga kura na ya uraia; malalamiko kuhusu upitishaji na uenguliwaji wa wagombea waliopitishwa kugombea nafasi mbalimbali katika uchaguzi huo; malalamiko kuhusu kukataliwa kibali cha kuangalia uchaguzi, hususan kwa upande wa mashirika yasiyo ya kiserikali; na wasiwasi kuhusu baadhi ya vifungu kwwenye kanuni za uchaguzi.

**19,681,259**
**Idadi ya watu waliondikiswa kupiga kura kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019**
**- TAMISEMI 2019**

Jambo kuu liliotia dosari uchaguzi huo ni kujitoa kwa wingi kwa vyama vinane (8) vya upinzani, vikiwemo vyama vikuu vya upinzani, kwa kile walichokiita kutotendewa kwa haki na juhudi za makusudi za kuwaondoa wagombea wao kwenye kinyang'anyiro. Vyama vya upinzani vilivyojitoa kweney uchaguzi huo ni ACT Wazalendo, CHADEMA, CUF, NCCR-Mageuzi, CHAUMA, CCK, UMD, NLD na UPDP. Chama cha ACT Wazalendo kilidai kwamba asilimia 96 ya wagombea wake walienguliwa, huku NCCR wakilalamika kwamba asilimia 90 ya wagombea wao walienguliwa. Kwa upande wa chama cha CHADEMA, idadi ya wagombea walionguliwa ni zaidi ya 1570. Kutokana na kuenguliwa na kujitoa huko, wagombea wengi wa chama tawala, CCM, walipita bila kupingwa, hivyo kupeleka uchaguzi kutofanyika katika maeneo mengi ya Tanzania Bara. Chama tawala kilishinda asilimia 95 ya viti bila kupigwa.




**Vyama vya siasa ambavyo wagombea wao walichukua fomu za kushiriki kwenye uchaguzi**

Kujitoa kwa vyama vingi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 ni doa kubwa katika demokrasia. Hatua hiyo iliwanyima watu nafasi ya kufurahia haki ya kupiga na kuibua maswali kuhusu uhalali wa mchakato mzima wa uchaguzi huo.







**Kesi ya Bob Chacha Wangwe kuhusu wakurugenzi wa jiji, manispaa, wilaya na miji kuwa wasimamizi wa uchaguzi**

Mwaka 2019 ulishuhudia pia maamuzi yaliyotolewa na Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa kuhusu vifungu vilivyo kweney Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ambavyo vinawaruhusu wakurugenzi wa jiji, manispaa, wilaya na miji kuwa wasimamizi wa uchaguzi. Mwezi Mei mwaka 2019, Mahakama Kuu ilitoa hukumu yake, ambayo ilisema kwamba vifungu hivyo vinakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, hivyo vifanyiwe marekebisho.

Hata hivyo, hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Rufaa mwezi Oktoba 2019 ilitengua maamuzi ya Mahakama Kuu na kuweka wazi kwamba wakurugenzi hao wanaweza kuwa wasimamizi wa uchaguzi. Kesi hiyo ya kikatiba ilifunguliwa mwaka 2018 na Bw. Bob Chacha Wangwe, ikionyesha wasiwasi kuhusu wakurugenzi hao kufanya kazi bila upendeleo wakiwa kama wasimamizi wa uchaguzi.

**Wito wa LHRC:**Hukumu iliyotolewa na Mahakama Kuu mwezi Mei 2019 ililenga kukidhi viwango vya uchaguzi vya kikanda na kimataifa ili kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki. Wakurugenzi kuendelea kuwa wasimamizi wa uchaguzi, kama ulivyoamuliwa na Mahakama ya Rufaa, kunaleta wasiwasi kuhusu uwezo wao wa kutosimama upande wowote pale wanapokuwa wasimamizi wa uchaguzi.

# SURA YA TATU: HAKI ZA KIJAMII, KIUCHUMI NA KIUTAMADUNI

**Utangulizi**

**Haki Zilizoangaliwa (4)**

**Haki ya Elimu, Haki ya Afya, Haki ya Kupata Maji Safi na Salama, Haki ya Kufanya Kazi**

Chini ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (ICCPR), mikataba mingine ya haki za binadamu na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Serikali ya Tanzania ina jukumu ya kuhakikisha utekelezaji wa haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kulingana na uwepo wa rasilimali. Haki hizi ni pamoja na haki ya elimu, haki ya afya, haki ya kupata maji safi na salama na haki ya kufanya kazi.

## 3.1. Haki ya Elimu

Kwa mwaka 2019, masuala makuu ambayo yaliathiri ufurahiaji na utekelezaji wa haki ya elimu ni pamoja na: utekelzaji wa sera ya elimu bila malipo; bajeti isiyotosheleza ya sekta ya elimu; upungufu wa matundu ya vyoo, madarsa, mabweni na vyumba vya kubadilishia nguo kwa ajili ya wasichana; upungufu wa walimu na nyumba za walimu; mimba za utotoni; uwezo wa kusoma na kuandika miongoni mwa wanafunzi katika baadhi ya shule; ukatili dhidi ya watoto; na utoro miongoni mwa walimu.

**Juhudi za serikali katika kuhakikisha utekelezaji wa haki ya elimu**

Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha utekelezaji wa haki ya elimu, ikiwemo kuendelea kutekeleza programu mbalimbali za sekta ya elimu na kutenda bajeti kwa ajili ya utekelzaji wa programu hizo, ukisimamiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na kuajiri walimu wapya, kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, pamoja na ujenzi na ukarabati wa majengo ya shule. Kwa upande wa mikopo ya elimu ya juu, jumla ya wanafunzi 49,485 walipewa mikopo.

Kwa mwaka 2019, Serikali iliendelea pia kutekeleza sera ya elimu bila ada, ambayo ilipelekea kuongezeka kwa upatikanaji wa elimu msingi (ambayo sasa ni mpaka Kidato cha Nne) na uandikishwaji wa wanafunzi wengi zaidi. Mamlaka mbalimbali za serikali katika ngazi za wilaya na kata ziliendelea kuhakikisha wazazi wanatii sheria ya elimu na kuwapeleka shule watoto au kuchukuliwa hatua za kisheria.

**Bajeti ya sekta ya elimu**

Kwa mwaka 2019, wadau wa elimu waliendelea kuelezea wasiwasi wao kuhusu bajeti inayotengwa kwa ajili ya elimu, ambayo haitoshelezi na haiendani na viwango vya kimataifa vya bajeti ya elimu, ikiwemo Tamko la Incheon la Utekelezaji wa Lengo la Maendeleo Endelevu namba 4. Suala jingine linalota wasiwasi ni ucheleweshaji wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya elimu na fedha hizo kutotolewa zote. Kwa mfano, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/19, hadi kufikia mwezi Machi 2019, fedha zilizowasilishwa wizarani zilikuwa ni asilimia 64.2 ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo na asilimia 73.1 kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Upungufu wa matundu ya vyoo, madarasa, mabweni na vyumba vya kubadilishia nguo kwa ajili ya wasichana**

Upungufu wa vyoo, madarasa pamoja na mabweni ni baadhi ya changamoto ambazo zimekuwa zikizikumba shule za serikali hasa kipindi hiki cha utekelezaji wa sera ya elimu bila ada, ambayo imepelekea kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi na hivyo kufanya huduma zilizopo kuwa hafifu zaidi.

Wakati kiwango cha rasmi cha uwiano wa vyoo na wanafunzi ukiwa ni choo kimoja kwa wanafunzi wa kike 20 (1:20) na choo kimoja kwa wanafunzi wa kiume 25 (1:25), uwiano wa wanafunzi kwa vyoo katika shule za msingi ni choo kimoja kwa wanafunzi 58, kwa mujibu matokeo ya utafiti uliofanywa na shirika la Twaweza, yaliyotolewa mwaka 2019. Jambo hili linahatarisha afya ya wanafunzi na kuathiri mazingira ya kujifunza kwa ujumla.

> Uwepo wa vifaa na huduma za maji, afya na usafi wa mazingira ni muhimu katika kuwafanya wasichana wabaki shuleni.

Changamoto nyingine katika shule za msingi na sekondari ni upungufu wa vifaa na huduma za maji, afya na usafi wa mazingira mashuleni, suala ambalo linawaathiri sana wanafunzi wa kike, hasa wanapokuwa katika hedhi. Changamoto hii ilendelea kuathiri mazingira ya kujifunza shuleni kwa upande wa toto wa kike, ambapo shule nyingi zilionekana kuwa na upungufu wa huduma hizi muhimu. Pamoja na mambo mengine, huduma hizi zinahitaji uwepo wa vyoo na vyumba vya kutosha vya kubadilishia nguo. Upungufu wa vyoo na vyumba hivyo huwafanya wasichana wawe na wakati mgumu wanapokuwa katika hedhi, hivyo kuwafanya wasichana kutokuwa huru wanapokuwa kwenye hali hiyo na wakati mwingine kuwalazimu kushindwa kabisa kwenda shuleni, hivyo kukosa masomo. Kutokuwepo kwa vyoo visafi na vya kutosha kunaathiri haki ya elimu ya watoto na kuchangia kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza kama vile kuhara na fangasi, jambo ambalo linachangia kuwafanya wanafunzi kuumwa na kushindwa kuhudhiria masomo mara kwa mara.

**Wito wa LHRC:** Serikali na wadau wengine kufanya juhudi za pamoja kutatua tatizo la upungufu wa vifaa na huduma za maji, afya na usafi wa mazingira mashuleni ili kuwafanya watoto wa kike kubaki shuleni. Huduma hizo ni pamoja na uwepo wa vyumba vya kubadilishia nguo kwa wasichana na upatikanaji wa pedi, sambamba na kupewa elimu kuhusu hedhi. Kushughulikia tatizo la upungufu wa matundu ya vyoo pia ni muhimu kwa wasichana mashuleni.

**Upungufu wa walimu na nyumba za walimu**

Upungufu wa walimu na nyumba za walimu pia ni changamoto inayoikumba sekta ya elimu nchini. Mwaka 2019, Serikali ilibainisha kuwa ili kutatua changamoto ya walimu nchini kuna uhitaji wa walimu 80,000. Kati ya maeneo yenye upungufu mkubwa wa walimu ni Wilaya ya Bumbuli mkoani Tanga na Wilaya ya Bukombe mkoani Geita.

**Changamoto ya umbali mrefu kufika shuleni**

Umbali mrefu kutoka na kuelekea shuleni uliendelea kutajwa kama mojawapo ya changamoto zinazoathiri utekelzaji wa haki ya elimu kwa watoto. Matukio kadhaa ya watoto kulazimika kutembea hadi kilomita 24 mpaka 30 kufika shuleni yaliripotiwa mwaka 2019 katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara, ikiwemo wilayani Siha mkaoni Kilimanjaro na wilayani Handeni na Muheza mkoani Tanga. Pia, umbali wa shule umeripotiwa kuwa ni mojawapo ya sababu za kushamiri kwa mimba za utotoni na wanafunzi wa kike kuacha shule. Pia, ni mojawapo ya changamoto zinazohatarisha maisha ya wanafunzi, hasa wa kike, kwa kuongeza hatari na uwezekano wa kufanyiwa ukatili wawapo njiani.

**Ongezeko la matukio ya walimu wa kiume kubaka na kuwapatia ujauzito wanafunzi wa kike**

Katika miaka ya hivi karibuni, kumeibuka wimbi la walimu wa kiume ambao huwafanyia ukatili wa kingono wanafunzi wa kike, ikiwemo ubakaji na kuingia nao katika mahusiano ya kimapenzi na kisha kuwapatia ujauzito. Hali hii inahatarisha ustawi wa mtoto wa kike na kuingilia haki yake ya kupata elimu bora. Kwa mujibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, kuanzia mwezi Julai mwaka 2016 jumla ya walimu 162 wamefukuzwa kazi kutokana na kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi wa kike mashuleni. Katika kipindi cha miaka ya 2018 na 2019, LHRC iliweza kukusanya jumla ya matukio 24 ya walimu waliohusishwa na ukatili wa kingono dhidi ya watoto, yaliyoripotiwa katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara. Walimu hao waliripotiwa kukamatwa au kukutwa na hatia na kufunguwa; na miongoni mwao ni walimu wakuu watatu.


**Ongezeko la mimba za utotoni, zinazopelekea watoto wa kike kuacha shule**

Katika kipindi cha miaka 2018 na 2019 pekee, LHRC ikusanya zaidi ya matukio ya mimba za utotoni 2,540. Kwa kuwa Serikali imeendelea kushikilia msimamo wake wa kutoruhusu wanafunzi wa kike wanaopata mimba kurudi shule, safari ya elimu ya wanafunzi hao mara nyingi hufika mwisho pindi wanapopata mimba, hivyo kukatisha ndoto zao.

Madereva bodaboda na walimu wa kiume wametajwa kama mojawapo ya wahusika wakuu wa mimba za utotoni mwaka 2019. Kwa upande wa madereva wa bodaboda, walisemekana kutumia mianya ya umbali wa shule na umaskini kuwarubuni wasichana kuanzisha mahuisano nao wa kimapenzi, huku walimu wa kiume wakitumia nafasi na nyadhifa walizonazo vibaya kuwarubuni wanafunzi wa kike na kutimiza azma zao.

**Ukatili dhidi ya watoto unapunguza utulivu na ufanisi shuleni**

Matukio mengi ya ukatili dhidi ya watoto yaliripotiwa mwaka 2019. Vitendo vya ukatili dhidi ya watoto kama vile kunyimwa chakula, kutukanwa matusi, unyanyasaji wa kingono, ubakaji, ulawiti, vitisho, udhalilishaji, na vipigo vinaweza kupelekea madhara ya kisaokolojia, kiakili na kimwili. Vitendo hivi pia vinaweza kupeleka mtoto kushindwa kujiamini, kuwa na msongo wa mawazo na kuathiri ustawi na utu wao, hivyo kupunguza utulivu na ufanisi wanapokuwa shuleni.




**Wasiwasi juu ya uwezo wa wanafunzi wa kusoma, kuandika na kuhesabu katika baadhi ya shule**

Mnamo mwezi Oktoba mwaka 2019, iliripotiwa mkoani Kilimanjaro kwamba wanafunzi 18 wa Kidato cha Kwanza na cha Pili katika mojawapo ya shule za secondary wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro walikuwa hawajui kusoma na kuandika. Jambo hili lilizua mjadala na wasiwasi kuhusu uwezo wa wanafunzi katika shule za msingi wa kusoma, kuandika na kuhesabu. Matokeo ya utafiti uliofanywa na shirika la Twaweza mashuleni mwaka 2017, yaliyotolewa mwaka 2019 yanathibitisha uwepo wa tatizo hili. Kwa mujibu wa matokeo hayo, wakati uwezo wa kusoma na kuandika katika Lugha ya Kiswahili ukiongezeka, uwezo wa kusoma na kuandika katika Lugha ya Kiingereza bado upo chini na unazidi kushuka. Wanafunzi wachache waliofikiwa na utafiti huo waliweza kusoma hadithi ya Darasa la Pili ya Kiingereza. Kwa upande wa Kiswahili, asilimia 62 ya wanafunzi wa Darasa la 3 waliweza kusoma hadithi ya Kiswahili, lakini asilimia 14 ya wanafunzi wa Darasa la Saba hawakuweza kusoma hadithi ya Darasa la Pili. Kwa upande wa Kiingereza, ni asilimia 15 ya wanafunzi wa Darasa la 3 na asilimia 47 ya wanafunzi wa Darasa la Saba pekee waliweza kusoma hadithi ya Kiingereza ya Darasa la Pili. Kwa upande wa uwezo wa kuhesabu, ufaulu katika zoezi la kuhesabu ulishuka kutoka asilimia 88 mwaka 2014 hadi asilimia 80 mwaka 2017.

Upungufu wa walimu, upungufu wa madarasa, kukosekana kwa chakula shuleni kwa ajili ya watoto, ushiriki mdogo wa wazazi, uwiano wa walimu na wanafunzi na upungufu wa vyoo na matundu vya vyoo ni changamoto ambazo zimeonekana kuathiri ubora wa elimu. Kwa upande wa ushiriki wa wazazi, utafiti wa hivi karibuni unaonyesha kwamba asilimia 50 ya wazazi hawashiriki ipasavyo katika kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni.

**Utoro miongoni mwa walimu**

Ripoti ya Benki ya Dunia kuhusu elimu na kujifunza ya mwaka 2018 inaonyesha kwamba utoro miongoni mwa walimu ni tatizo kubwa katika nchi za Afrika Mashariki, ikiwemo Tanzania. Ripoti hiyo inaonyesha kwamba muda mwingi wa masomo kupotea; na kwa upande wa Tanzania ni asilimia 55 tu ya muda uliopangwa kwa ajili ya kufundisha ndio hutumiwa na walimu kufundisha. Utoro huu wa walimu huathiri mchakato wa watoto kujiufunza na kupunguza ufanisi na uelewa darasani. Kwa mujibu wa ripoti hiyo, barani Afrika mara nyingi walimu wanakuwa hawapo shuleni au wanakuwepo shuleni lakini hawapo darasani.

Kwa mwaka 2019, tatizo la utoro miongoni mwa walimu lilibuka tena katika mjadala nchini Tanzania. Mnamo mwezi Novemba 2019, Tume ya Utumishi wa Walimu ilibainisha kwamba tangu tume hiyo ianzishwe mwezi Julai mwaka 2016, imepokea malalamiko 7,123 kuhusu walimu, ikiwemo yanayohusiana na utoro, kukiuka maadili na kujihusisha katika mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi wa kike. Malalmiko mengi (asilimia 76) yalikuwa ni ya utoro miongoni mwa walimu.

**Sifa za kuajiriwa miongoni mwa wahitimu wa elimu ya juu**

Changamoto ya wahitimu wengi wa elimu ya juu kukosa sifa za kuajiriwa iliibuka tena mwaka 2019. Katika kipindi cha mwaka huu, iliripotiwa kwamba takribani asilimia 45 ya wahitimu wa elimu ya juu waliosomea TEHAMA hawana sifa za kuajiriwa na uzoefu wa kuwawezesha kuajiriwa katika sekta hiyo ya TEHAMA ambayo inaendelea kuwa na ushindani mkubwa. Waajiri waliendelea kuonyesha wasiwasi kuhusu ubora wa elimu ambayo wahitimu wanapata katika vyuo na vyuo vikuu, wakilalamika kwamba wanalazimika kutumia fedha nyingi kuwapatia mafunzo wahitimu wanaojiriwa ili kuimarisha uwezo wao wa kufanya kazi. Katika kusaidia kutatua tatizo hili, mwezi Juni mwaka 2019, kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) ilianzisha mabaraza ya ujuzi ya kisekta, ambayo yalizinduliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mh. Prof. Joyce Ndalichako.

## 3.2. Haki ya Afya

Kwa mwaka 2019, Serikali iliendelea kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha utekelezaji wa haki ya afya kulingana na rasilimali zilizopo. Hatua hizo ni pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya programu mbalimbali katika sekta ya afya zinazolenga kuboresha huduma za afya, ujenzi na ukarabati wa hospitali na na vituo vya afya; usambazaji wa madawa muhimu na vifaa tiba; na kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya zinazohusiana na VVU.

Hata hivyo, kama ilivyo kwa upande wa haki ya elimu, changamoto kubwa katika utekelezaji madhubuti wa programu za sekta ya afya imeendelea kuwa bajeti inayotengwa kwa ajili ya sekta hiyo, ambayo haitoshelezi. Changamoto nyingine ni pamoja na fedha za bajeti kutowasilishwa zote kama zilizvyotengwa na kuchelewa. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2018/19, ni asilimia 39 ya fedha za bajeti zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilikuwa imewasilishwa kufikia mwezi Machi 2019.

Changamoto nyingine ni upungufu wa watumishi, ambapo sekta ya afya iliendelea kukumbwa na changamoto ya upungufu wa watumishi, hasa madaktari. Kwa mujibu wa mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO), daktari mmoja anatakiwa kuhudumia wagonjwa wasiozidi 10,000 kwa mwaka, lakini nchini Tanzania daktarin mmoja anahudumia mpaka wagonjwa 22,000 kwa mwaka.

Changamoto nyingine zilizoathiri ufurahiaji wa haki ya afya ni pamoja na upungufu wa vyoo katika baadhi ya maeneo ya Tanzania Bara na upungufu wa majengo na vitanda hospitalini na kwenye vituo vya afya. Mathalani, iliripotiwa kwamba jumla ya kaya 22,547 mkoani Mara hazikuwa na vyoo. Jambo hili ni hatari, kwani linasababisha kusambaa kwa urahisi kwa magonjwa ya mlipuko, ikiweo kipindupindu na kichocho. Katika kupambana na tatizo hili, Serikali iliendelea kutekeleza kampeni ijulikano kama Usichukulie Poa, Nyumba ni Choo.  Uhaba wa majengo na vitanda katika hospitali na vituo vya afya uliripotiwa katika maeneo ya Igunga mkoani Tabora, Sumbawanga mkoani Rukwa na Kinondoni mkoani Dar es Salaam. Upungufu huu unaathiri utoaji wa huduma bora za afya, ikiwemo baadhi ya wagonjwa kulazimika kutumia kitanda kimoja na wengine kulala chini.

Katika kipindi cha mwaka 2019, tatizo la afya ya akili na matukio ya watu kujiua yalichangia kuhatarisha haki ya afya. Iliripotiwa kwamba jumla ya Watanzania 666 walijiua katika kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi 2019. Hii ni sawa na wastani wa watu 14 waliojiua kila mwezi. Kwa mwaka 2019, kulikuwa na matukio 105 ya watu kujiua kwa kujinyonga, matukio 8 ya kujiua kwa kunywa sumu na matukio 2 ya kujiua kwa kujipiga risasi. Sababu za watu kujiua ni pamoja na mahusiano ya kimapenzi (wivu wa kimapenzi), migogoro ya kifamilia, matatizo mahala pa kazi na ugumu wa maisha. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani, takribani watu 800,000 duniani hufa kila siku sababu ya kujiua. Asilimia 79 ya matukio ya kujiua duniani kote yanatokea katika nchi zenye uchumi wa kati. Pia, utafiti unaonyesha kwamba wanaume wanajiua zaidi ukilinganisha na wanawake. Changamoto kubwa katika kushughulikia tatizo la watu kujiua ni pamoja na: unyanyajpaa, ambao huwakatisha tamaa watu wanoafikiria kujiua kutafuta msaada; kukosekana kwa programu madhubuti za kuzuia watu kujiua; na mapungufu katika taarifa na takwimu kuhusu kujiua.

Changamoto nyingine iliyoonekana kuathiri haki ya afya mwaka 2019 ni kuongeza kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Kama inavyoelezewa katika Sura ya Tano ya Muhtasari huu wa Ripoti ya Haki za Binadamu, vitendo vya ukatili dhidi ya watoto nchini Tanzania, hasa ubakaji na ulawiti, vimekuwa vikiongezeka kwa kasi, hususan katika miaka ya hivi karibuni ya 2018 na 2019. Vitendo hivi vina madhara makubwa kwa watoto, vikiathiri kwa kiasi kikubwa afya yao ya akili. Watoto ambao hawawezi kufikia kirahisi huduma za wahanga wa ukatili, ikiwemo ushauri nasaha, wapo katika hatari zaidi ya kuathirika kiakili.

### 3.3. Haki ya kupata Maji Safi na Salama

Haki ya kupata maji safi na salama ni haki muhimu ya kiuchumi na kijamii, ambayo inatakiwa kutekelezwa kila siku. Tafiti za hivi karibuni zinaonyesha kwamba takribani asilimia 60 ya Watanzania wanapata huduma ya maji; na iliripotiwa kwamba hatua mbalimbali zilichukuliwa na Serikali mwaka 2019 kuimarisha haki ya maji, ikiwemo kuanzisha Jukwaa la Kitaifa la Wadau wa Sekta Mtambuka katika Usimamizi wa Rasilimali za Maji, na utekelezaji wa Mipango ya Usalama wa Maji.

Kwa mwaka 2019, changamoto mbalimbali ziliendelea kuathiri upatikanaji wa maji safi na salama. Changamoto kubwa ni kwa upande wa bajeti, ambayo haitoshelezi na haifikii viwango vya kimataifa vya bajeti ya maji. Changamoto nyingine ni fedha zilizotengwa kutowasilishwa kikamilifu na kuchelewa. Kwa mfano, hadi kufikia mwezi Aprili mwaka 2019, Wizara ya Maji ilikuwa imepokea asilimia 51 tu ya bajeti iliyotengwa kwa ajli ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2018/19, hivyo kuathiri utekelezaji madhubuti wa miradi mbalimbali ya maji. Changamoto nyingine zilizoikabili sekta ya maji kwa mwaka 2019 ni pamoja na: uhaba wa wataalamu katika sekta hiyo; kushindwa kutekeleza na kukamilisha miradi ya maji kwa muda na ufanisi unaotakiwa; malimbikizo ya bili za maji kwa upande wa taasisi za serikali; uwekezaji mdogo wa sekta binafsi kwenye miradi ya maji; upotevu wa maji; miradi ya maji kukosa uendelevu; na changamoto zinazozikumba Bodi za Maji za Mabonde kama vile uhaba wa fedha, uhaba wa wataalamu na uhaba wa vifaa.

- Upungufu wa wataalamu katika sekta ya maji ni asiimia 38.
- Katika kipndi cha kuanzia mwaka 2016 hadi 2019, mamlaka za maji za mikoa zilipoteza wastani wa Shilingi Bilioni 51 kwa mwaka, sawa na upotevu wa maji wa asilimia 33.
- Kufikia mwezi Aprili mwaka 2019, taasisi za serikali zilikuwa zinadaiwa bili za maji zenye jumla ya thamani ya Shilingi Bilioni 21.84

### 3.4. Haki ya Kufanya Kazi

Haki ya kufanya kazi inajumuisha haki ya kupata kipato kwa kufanya kazi na haki ya mazingira mazuri ya kufanyia kazi. Kwa mwaka 2019, haki ya kufanya kazi iliathiriwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo tatizo la ukosefu wa ajira na ukosefu wa sifa za kuajiriwa; malimbikizo ya madai ya mishahara na likizo, hususan kwa walimu; makato mbalimbali, ukiacha ya kodi ya mshahara; upungufu wa wafanyakazi katika sekta muhimu za afya, elimu na maji; mazingira duni ya kufanyia kazi; na ukiukwaji wa haki za wafanyakazi, hususan kwa wafanyakazi katika makampuni na viwanda binafsi.

- Tatizo la wahitimu wengi wa elimu ya kuu kuonekana kukosa sifa za kuajiriwa kupelekea kuundwa kwa mabaraza ya kukuza sifa hizo yaliyozinduliwa mwaka 2019. Tafiti za mwaka 2014 za Baraza la Afrika Mashariki la Vyuo Vikuu zilionyesha kwamba zaidi asilimia 50 ya wahitimu wa elimu ya juu hawana sifa za kuajiriwa zinazotakiwa katika soko la ajira, ambalo lina ushindani mkubwa.

Kwa mwaka 2019, iliripotiwa kwamba asilimia 45 ya wahitimu wa kozi ya TEHAMA hawana sifa na uzoefu wa kuwawezesha kuajiriwa. Waajiri wengi wamekuwa hawaridhishwi na kiwango cha ujuzi walionao wahitimu na hivyo kuweka vigezo vigumu vya kuajiriwa, ikiwemo uzoefu wa miaka mingi. Jambo hili liliendelea kuwaathiri vijana wengi walioendelea kutafuta kazi mwaka 2019, hivyo kuwafanya kushindwa kufurahia na kutekeleza haki yao ya kufanya kazi.

- Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka wa fedha 2017/18 pia imeo nyesha kuwepo kwa tatizo la madai ya malimbikizo ya mishahara na likizo ya wa tumishi katika halmashauri 22. Kwa mwaka 2019, madai ya walimu ya malimbikizo ya mishahara na likizo yaliibuliwa kama changamoto katika ufurahiaji wa haki ya kufan ya kazi kwa upande wa walimu. Kwa mujibu wa Naibu Waziri wa Wizara ya TAMISEMI, Serikali inadaiwa malimbikizo ya mishahara na likizi na jumla ya walimu 86,000 nchini. Alielezea kwamba walimu hao wanadai jumla ya Shilingi bilioni 43, ambazo zinajumuisha malimbikizo ya mishahara na likizo. Madai ya watumishi wa umma yanaweza kuathiri morali ya ufanyaji kazi, hivyo kuathiri utoaji wao wa huduma katika jamii, ikiwemo huduma za elimu na afya. Hivyo basi, ni muhimu Serikali ikafa nyia kazi changamoto hii na kuwalipa watumishi wote wanaodai malimbikizo ya mishahara na likizo ili kuwapa motisha ya kundelea vizuri na kazi zao.

- Kwa mwaka 2019, wafanyakazi na watumishi waliendelea kuelemewa na mzigo wa kodi ya mshahara na makato mengine ambayo wafanyakazi wanakatwa. Sheria ya Urejeshaji Madeni ya mwaka 1970 inatamka kwamba wafanyakazi wasilipowe chini ya theluthi moja ya mshahara baada ya makato, lakini utekelezaji wa sheria hii ume kuwa ni changamoto kutokana na makato kuonekana kuzidi kama ilivyobainishwa katika Ripoti ya Mkaguzi wa Serikali ya mwaka waf edha 2016/17 iliyotoka mwaka 2018. Mojawapo ya changamoto zilizochangia hali hi ini makato ya mkopo wa elimu ya juu ya asilimia 15 ya mshahara – ambayo yalipanda kutoka asilimia 8 kuanzia mwezi Januari mwaka 2017. Kodi ya mshahara ni asilimia 30 ya mshahara, huku kukiwa bado kuna makato mengine kama ya hifadhi ya jamii na mikopo mingine ambayo watumishi wamekopa. Kuzidi kwa makato katika mishahara kunaweza kuwasababisha wafanyakazi kutofanya kazi kwa morali na kwa weledi, na hivyo k uathiri utoaji huduma kwa jamii.

- Upungufu wa watumisihi katika sekta za afya, maji na elimu umeleta changamoto ya kuzidiwa na kazi kwa upande wa watumishi waliopo, jambo ambalo linaathiri ufanisi katika utendaji kazi na haki zao za msingi kama vile haki ya kupata muda wa kutosha wa kupumzika na haki ya afya. Hii ni kwa sababu wafanyakazi waliopo wa nalazimika kufanyaka kazi zaidi ili kuweza kufikia malengo yaliyowekwa.

- Mazingira duni ya kufanyika kazi yaliathiri pia ufurahiaji na utekelezaji wa haki ya kufanya kazi mwaka 2019. Changamoto hii ilionekana kuwa kubwa zaidi katika sekta za elimu na afya. Ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kuhusu haki za

binadamu na biashara ya mwaka 2018/19 pia inaonyesha kwamba mazingira duni ya kazi ilikuwa changamoto katika ufurahiaji wa haki ya kufanya kazi kwa wanafanykazi katika makampuni na viwanda binafsi, ikiwemo kutopatiwa vifaa vya kazi.

o Ukiacha changamoto ya mazingira duni ya kufanya kazi, Ripoti ya Haki za Binadamu na Biashara ya mwaka 2018/19 ilionyesha kwamba haki za wafanyakazi katika makampuni binafsi ziliendelea kukiukwa kwa namna mbalimbali, ikiwemo: ujira mdogo/usiotosheleza; uminyaji wa uhuru wa kujumuika; ukiukwaji wa makubaliano ya mkataba; kunyimwa nakala za mkataba wa kazi; kutolipwa kwa kazi inayofanyika baada ya muda wa kawaida wa kazi; kutopatiwa muda wa kutosha wa kupumzika; na ubaguzi wa wanawake na watu wenye ulemavu.

# SURA YA NNE: HAKI ZA KIUJUMLA

**Haki Zilizoangaliwa (4)**

**Haki ya Maendeleo, Haki ya Kufurahia na Kufaidika na Maliasili**

Haki za Kiujumla ni haki ambazo zinafurahiwa na watu wengi. Haki hizi ni pamoja na Haki ya Maendeleo na Haki ya Kufurahia na Kufaidika na Maliasili.

## 4.1. Haki ya Maendeleo

Haki hii inajumuisha ushiriki katika kuchangia na kufurahia maendeleo ya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa.

**Mwelekeo chanya kwenye kuendeleza miundombinu, ishara ya kupiga hatua katika utekelezaji wa haki ya maendele**o

Kwa mwaka 2019, Serikali iliendelea kutekeleza miradi mbalimbali iliyolenga kuimarisha miundombinu katika sehemu mbalimbali za Tanzania, hususan Tanzania Bara. Miradi hiyo ni pamja na ujenzi wa madaraja na barabara za juu, upanuzi wa barabara na ujenzi wa barabara mpya, hasa maeneo ya vijijini. Taasisi muhimu katika kushungulikia maendeleo ya miundombinu ni pamoja Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA). Jijini Dar es Salaam, LHRC iliweza kushuhudia utekelezaji wa miradi ya miundombinu kama vile Barabara za juu na chini za Ubungo, ujenzi wa Daraja la Salender, upanuzi wa barabara ya Morocco-Mwenge na upanzui wa barabara ya Kimara-Kibaha.

**Wasiwasi kuhusu maendeleo ya kibinadamu na maendeleo ya kisiasa**
Pamoja na kupiga hatua katika maendeleo ya kiuchumi, kasi ya maendeleo ya kibinadamu imeendelea kuwa changamoto. Changamoto kubwa bado ni namna gani maendeleo hayo yanapunguza umaskini ili kuleta maendeleo ya kibinadamu. Bado watu wengi nchini ni maskini, wakiishi chini au juu kidogo ya Dola moja ya Kimarekani. Kuwekeza zaidi kwenye sekta ya kilimo, ambayo ndiye mwajiri mkuu, ni jambo la muhimu katika kukuza uchumi na kutokomeza umaskini. Hivyo basi, kuna haja ya Serikali kuongeza bajeti ya sekta ya kilimo ili kulinda haki ya maendeleo.

Kwa upande wa haki za kisiasa, changamoto kubwa ilikuwa uminyaji wa haki za ushiriki. Maendeleo ya kisiasa yanategemea ufurahiaji na utekelezaji wa haki za ushiriki, ambazo ni pamoja na uhuru wa kujieleza, uhuru wa kukusanyika na uhuru wa kujumuika, lakini kama ilivyoelezewa kwenye Sura ya Pili hapo juu, ufurahiaji na utekelezaji wa haki za ushiriki uliendelea kudorora mwaka 2019.

**Maendeleo ya kijamii**
Kama ilivyoelezewa katika Sura ya Tatu hapo juu, hatua kadhaa zilichukuliwa Serikali na wadau wengine kutekeleza haki za kijamii, ikiwemo haki ya elimu, haki ya afya na haki ya maji safi na salama kwa mwaka 2019. Hata hivyo, changamoto mbalimbali ziliendelea kuathiri utekelezaji wa haki hizi za msingi, ikiwemo upungufu wa bajeti na upungufu wa wafanyakazi katika sekta hizo. Pamoja na changamoto hizi, suala la muhimu la kukumbuka ni kwamba ukusanyaji wa mapato/kodi ni muhimu sana katika utekelezaji wa haki hizi za kijamii na kiuchumi, ambazo hutekelezwa kulingana na uwepo wa rasilimali.

## 4.2. Haki ya Kufurahia na Kufaidika na Maliasili
Kwa mwaka 2019, hatua mbalimbali zilichukuliwa na Serikali kukuza haki ya kufurahia na kufaidika na maliasili. Hatua hizi ni pamoja utekelzaji wa sheria kulinda maliasili; kuongeza ufuatiliaji wa makampuni katika sekta ya uchimbaji – hususan sekta ya madini; na kuchukua hatua mbalimbali kushughulika suala la ukwepaji kodi, ikiwemo dhidi ya Kampuni ya Uchimbaji Madini ya Acacia, ambayo imekuwa ikihusishwa na vitendo vya rushwa na ukwepaji kodi katika miaka ya hivi karibuni, ikiwemo mwaka 2019.

**Changamoto katika utekelezaji na ulinzi wa haki ya kufurahia na kufaidika na maliasili**
Changamoto mbalimbali ziliendela kuathiri utekelezaji Madhubuti wa haki ya kufurahia na kufaidika na maliasili mwaka 2019. Changamoto hizi ni pamona na rushwa, ukwepaji kodi, misahamaha ya kodi, na mianya katika sheria za madini na maliasili.

# SURA YA TANO: HAKI ZA MAKUNDI MAALUM

**Makundi Yaliyoangaliwa (5)**

**Wanawake, Watoto, Watu wenye Ulemavu, Wazee, Watu wanaoishi na VVU**

Haki za msingi za makundi maalum ambazo huwa zinavunjwa mara nyingi ni **Haki dhidi ya Ukatili, Haki ya Usawa na Kutobaguliwa, na Haki ya Kupata Huduma Bora za Kijamii.**

## 5.1. Haki za Wanawake

Ukiacha mikataba mbalimbali ya haki za binadamu inayotoa ulinzi wa haki za wanawake kwa watu wote, kuna mikataba kadhaa ambayo ni ya haki za wanawake pekee. Mikataba hii ni pamoja na Mkataba wa Kuondoa Aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) wa mwaka 1979 na Mkataba wa Afrika wa Haki za Wanawake (Maputo Protocol). Jambo kubwa linalokatazwa katika mikataba hii ni ubaguzi dhidi ya wanawake unaopelekea kushindwa kufurahia haki zao muhimu kama binadamu.

Kwa mwaka 2019, ulinzi wa haki za wanawake uliathiriwa zaidi ya vitendo vya ukatili, hasa ukatili wa kimwili na kingono.

**Hatua zilizochukuliwa na Serikali, asasi za kiraia na wadau wengine kukabiliana/kupambana na ukatili dhidi ya wanawake**

Wadau mbalimbali wa kiserikali na wasio wa kesrikali waliendelea na juhudi mbalimbali kupambana na ukatili dhdi ya wanawake, ikiwempo kupitia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kuondoa Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto; kuboresha upatikanaji na ufikiaji wa msaada wa kisheria kwa makundi totauti, yakiwemo wanawake; ukamataji na ufunguaji wa mashtaka dhidi ya watuhumiwa wa ukatili dhidi ya wanawake; kuimarisha uwezo wa madawati ya jinsia na watoto ya Jeshi la Polisi; na kuendelea kutekeleza programu mbalimbali za kuwainua na kuwawezesha wanawake. Juhudi hizi ni muhimu sana katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu kuhusiana na usawa wa kijinsia na afya, pamoja na lengo la maisha bora chini ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025

.


Kuongezeka kwa utoaji taarifa kuhusu matukio ya ukatili dhidi ya wanawake
Juhudi za pamoja za kupambana na ukatili dhidi ya watoto na wanawake, ikiwemo Serikali na wadau wengine nje ya Serikali, zimesaidia kuongezeka kwa utoaji taarifa kuhusu matukio ya ukatili dhidi ya wanawake.

88,612+
Idadi ya matukio ya ukatili wa kijinsia yaliyoripotiwa polisi kuanzia mwaka 2017 hadi mwezi Juni 2019

**Idadi kubwa ya matukio ya ukatili dhidi ya wanawake**
Pamoja na juhudi mbalimbali zilizofanywa na kuendelea kufanywa, ukatili dhidi ya wanawake, hususan ukatili wa kimwili na kingono, umeendelea kuwa kikwazo kikuu katika ufurahiaji na utekelezaji wa haki za wanawake nchini Tanzania.

Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2017 hadi mwezi Juni 2019, jumla ya matukio 88,612 ya ukatili wa kijinsia yameripotiwa katika vituo mbalimbali vya polisi. Kwa mwaka 2019, katika kipindi cha mwezi Januari hadi mwezi Juni 2019, jumla ya matukio 3,709 ya ubakaji wa wanawake na watoto yaliripotiwa katika vituo vya polisi nchini.

Mkoani Kigoma, mwaka 2019 pia ulikuwa wenye changamoto kubwa kwa wanawake ambao walifanyiwa ukatili wa kingono na kikundi cha wabakaji kilichojiita 'Teleza.' Taarifa mbalimbali na uchunguzi uliofanywa na LHRC na wadau wengine vinaonesha kwamba kikundi hichi cha wabakaji kilikuwa kinawavamia wanawake katika nyumba wanazoishi kisha kuwabaka, na wanawake wengine walibakwa zaidi ya mara moja. Kiongozi wa kikundi hicho alikamatwa mwezi Juni mwaka 2019.




**Matukio ya ukatili wa kijinsia yaliyoripotiwa polisi miaka ya 2017 & 2018 (n=84,903)**

Kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Madawa ya Kulevya na Uhalifu (UNODC), nyumbani pamekuwa sehemu hatari zaidi kwa wanawake. Ripoti iliyotolewa na shirika hilo mwaka 2019 inaonyesha kwamba zaidi ya wanawake 1500 barani Afrika huuwawa na wenzi wao na familia zao. Zaidi ya 50% ya wanawake duniani huuwawa na wenzi wao au wanafamilia. Asilimia 35 ya wanawake huuwawa na wenzi wao.

**1583**
Wastani wa wanawake waliouawa na wenzi wao na wanafamilia kila mwezi barani Afrika mwaka 2017.

Nchini Tanzania, LHRC ilikusanya matukio 14 ya ukatili wa kimwili dhidi ya wanawake kwa mwaka 2019, ambapo matukio 12 yalipelekea vifo vya wanawake hao. Kati ya mauaji 12 ya wanawake hao, 8 yalisababishwa na wivu wa kimapenzi. Hata hivyo, LHRC haikufanikiwa kupata idadi ya matukio yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi, ambayo huwa ni mengi zaidi.

**Ubaguzi wa wafanyakazi wanawake mahala pa kazi**
Mwaka 2019, Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) mkoani Morogoro kiliripoti kwamba kilipokea malalamiko kutoka katiak vituo binafsi vya afya na hospitali kuhusu wafanyakazi wanawake kubaguliwa, hasa wale ambao ni wajawazito. Ripoti ya Haki za Binadamu na Biashara ya mwaka 2018/19 illiyoandaliwa na LHRC pia inaonyesha kwamba wanawake wanaendelea kuwa wahanga wa aina mbalimbali za ubaguzi wa kijinsia mahala pa kazi, ikiwemo kufukuzwa kazi bila kufuata utaratibu. Mathalani, mkoani Mtwara ilielezewa kwamba masuala kama mimba, hedhi na unyonyeshaji ni mojawapo ya sababu waajiri wengi viwandani wanasita kuajiri wanawake. Ripoti ya Haki za Binadamu na Biashara pia inaonyesha uwepo wa ubaguzi dhidi ya wanawake katika sekta ya madini. Utafiti zaidi unahitajika kufanyika ili kubaini ukubwa wa tatizo la ubaguzi dhidi ya wanawake mahala pa kazi.

**Rushwa ya ngono katika ajira, taasisi za elimu ya juu na siasa**
Rushwa ya ngono, hasa katika ajira, mahala pa kazi, katika taasisi za elimu ya juu na katika siasa iliibuliwa kama mojawapo ya changamoto kubwa kwa upande wa wanawake. Ripoti ya hivi karibuni ya Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) inaonesha kwamba takribani asilimia 89 ya wanawake katika sekta ya umma wamewahi kufanyiwa ukatili wa kingono wakati wa kutafuta kazi, kupandishwa cheo au kupata huduma. Tasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) iliripoti kwamba inapanga kushirikiana na wadau wengie kufanya utafiti kuhusu rushwa ya ngono katika maeneo na sekta mbalimbali, ikianzia kwenye taasisi za elimu ya juu.

**Ukatili wa kijinsia na ufikiaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030**
Kuongezeka kwa matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na wasichana kunahatarisha juhudi za Serikali na wadau wengine za kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu yanayohusiana na usawa wa kijinsia.

**Bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kuondoa Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto 2017/2022**
Uchambuzi wa bajeti iliyotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kuondoa Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2019/20 unaonyesha kwamba bajeti inayotengwa haikidhi mahitaji, jambo linaloathiri juhudi za kuondoa ukatili dhidi ya wanawake na watoto. Uchambuzi unaonyesha kwamba japokuwa bajezi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iliongezeka kwa asilimia 10.7 kwa mwaka 2019/20 ukilinganisha na mwaka 2018/19, bajeti kwa ajili ya Idara ya Maendeleo ya Jamii ilipungua kwa asilimia 1.9, huku bajeti ndogo kwa ajili ya Kitengo cha Ustawi wa Jamii, ambacho kipo chini ya Idara ya Maendeleo ya Jamii, ikipungua kwa asilimia 19.3.

## 5.2. Haki za Watoto

Haki za watoto zinalindwa katika mikataba mikubwa miwili ya haki za watoto, ambayo ni: Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (CRC) wa mwaka 1989 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) wa mwaka 1990, yote ikiwa imeridhiwa na Tanzania. Kwa hapa nchini Tanzania pia tuna Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 ambayo inataja haki za msingi za mtoto kama zilivyoelezewa kwenye mikataba hiyo na kueleza wazi kwamba katika kufanya maaumuzi yoyote kuhusu mtoto **kanuni ya maslahi bora ya mtoto** lazima izingatiwe. Mikataba hii na sheria ya mtoto inatoa wajibu kwa Serikali, wazazi, walezi na wanajamii kwa ujumla kuwalinda watoto dhidi ya vitendo vyote vya ukatili na ubaguzi.

Kwa mwaka 2019, uhuru dhidi ya ukatili ulendelea kuwa haki ya watoto inayokikukwa zaidi, ikisababishwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto. Matokeo makuu yafuatayo kuhusiana na haki ya ukatili dhidi ya watoto yalipatikana mwaka 2019:

**Juhudi za Serikali, Mhimili wa Mahakama na Asasi za Kiraia katika Kuzuia na Kupambana na Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto**
Kwa mwaka 2019, juhudi mbalimbali zilizofanywa na Serikali, Jeshi la Polisi, Mahakama na asasi za kiraia zilichangia utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto. Hatua hizo ni pamoja na kueneza uelewa kuhusu ukatili dhidi ya watoto; ukamataji na ufunguaji wa mashtka dhidi ya watuhumiwa wa vintendo vya ukatili; utoaji wa msaada wa kisheria; kufanya uchechemuzi; kukusanya matukio ya ukatili yaliyoripotiwa kwa ajili ya kufanyia uchechemuzi; utoaji wa huduma za kisheria, kiafya na huduma nyingine kwa wahanga wa ukatili na familia zao; na utungaji wa kanuni za kuharakisha usikilizaji wa mashauri zinazohusisha watu walio katika makundi maalum, ikiwemo watoto.

**Kuongezeka kwa utoaji taarifa kuhusu matukio ya ukatili dhidi ya watoto**

Juhudi za pamoja za wadau wa kiserikali na wasio wa kiserikali za kupambana na ukatili dhidi ya watoto na wanawake mwaka 2019 zilisaidia kuongezeka kwa utoaji taarifa kuhusu matukio ya ukatili dhidi ya watoto miongoni mwa wanajamii.

42,824+
Idadi ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyoripotiwa polisi, 2016 - 2019

**Ukatili wa kimwili dhidi ya watoto**

Matukio ya ukatili wa kimwili yaliendelea kuwa changamoto katika ufurahiaji na utekelezaji wa haki za watoto mwaka 2019, japokuwa matukio machache zaidi yaliripotiwa na kukusanywa na LHRC ukilinganisha na mwaka 2018. Asilimia 16 ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyoripotiwa yalikuwa ni ya ukatili wa kimwili.

Mwaka 2019 ulishuhudia matukio ya mauaji ya kikatili ya watoto mkoani Njombe, ambayo yalianza mwishoni mwa mwaka 2018 na hadi mwanzoni mwa mwaka 2019, jumla ya watoto kumi waliuwawa kikatili, huku miili ya baadhi yao ikikutwa bila baadhi ya viungo vya mwili, ikiwemo sehemu za siri. Mauaji haya yaliripotiwa kuhusishwa na imani za kishirikina.


Ukatili wa kimwili dhidi ya watoto hupelekea watoto kupata majeraha mbalimbali katika miili yao, yakiwemo majeraha ya kudumu, kupata ulemavu, na hata kufariki. Katika kipindi cha Januari hadi Disemba mwaka 2019, LHRC ilikusanya jumla ya matukio 26 ya ukatili dhidi ya watoto yaliyopelekea vifo vya watoto hao.

**Kuongezeka kwa matukio ya ukatili wa kingono dhidi ya watoto katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara**

Katika kipindi cha mwezi Januari hadi Juni mwaka 2019, jumla ya matukio 3,709 ya ubakaji yaliripotiwa polisi, ambayo ni matukio 126 zaidi ya yale yaliyoripotiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Pia, katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya mwaka 2019, jumla ya matukio 688 ya ulawiti yaliripotiwa katika vituo vya polisi, ambayo ni matukio 141 zaidi ya yale yaliyoripotiwa mwaka 2018.

Kupitia vyombo vya habari, LHRC ilibaini kwamba asilimia 84 ya matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliyoripotiwa na vyombo vya habari mwaka 2019 ni ya ukatili wa kingono. Matukio hayo yaliropotiwa katika mikoa ya Tabora, Njombe, Geita, Songwe, Simiyu, Pwani, Ruvuma, Kilimanjaro, Katavi, Mara, Dodoma, Kagera, Mwanza, Iringa, Mbeya, Lindi, Manyara, Arusha Morogoro, Tanga, Singida, Rukwa na Dar es Salaam. Matukio ya ukatili wa kingono yaliyoripotiwa ni pamoja na ubakaji wa mande wa msichana wa Darasa la Saba katika Shule ya Msingi Mahina jijini Mwanza. Msichana huyo alibakwa hadi kufa. Vitendo vingi vya ukatili dhidi ya watoto hufanywa nyumbani, mitaani na shuleni.


**% ya matukio ya ukatili wa kingono na kimwili dhidi ya watoto yaliyoripotiwa na vyombo vya habari mwaka 2019 (N=319)**
Chanzo: Utafiti wa vyombo vya habari wa LHRC 2019





162 Idadi ya walimu waliofukuzwa kazi na Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kujiingiza katika mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi wa kike tangu mwaka 2016.

Kwa mwaka 2019, walimu wa kiume, madereva bodaboda na wazazi wa kiume walitajwa kuwa miongoni mwa watuhumiwa wakuu wa ukatili wa kingono dhdi ya watoto. Walimu wa kiume wanaendelea kutajwa kuhusika na vitendo mbalimbali vya ukatili dhidi ya watoto, ikiwemo kubaka wanafunzi na kuwapatia ujauzito. Katika kipindi cha mwaka 2018 hadi 2019, LHRC ilikusanya jumla ya matukio 24 ya walimu kutajwa kuhusika na ukatili wa kingono dhidi ya watoto, ambao ama walikamatwa kama watuhumiwa au kupelekwa mahakamani na kukutwa na hatia. Kati ya kesi hizi, kesi tatu zinawahusu walimu wakuu.

Changamoto zinazoathiri mapambano dhidi ya ukatili dhidi ya watoto ni pamoja na kutembea umbali mrefu kwenda na kutoka shule, ambako kunachangia kuwaweka watoto, hasa wasichana, katika hatari kubwa zaidi ya kufanyiwa vitendo vya ukatili, hasa ubakaji na ulawiti; kasi ndogo ya uchunguzi na uendeshaji wa mashtaka dhidi ya watuhumiwa wa ukatili dhidi ya watoto; tabia ya wazazi, wanafamilia na wanajamii kwa ujumla kupendelea kumaliza kesi za ukatili dhidi ya watoto kupitia 'kikao cha familia' ili 'kuficha aibu ya familia;' wazazi au wanafamilia kumshurutisha mtoto ambaye ni mhanga wa ukatili kutotoa ushahidi dhidi ya mtuhumiwa au kutoa ushahidi wa uongo; uelewa mdogo kuhusu upatikanaji wa haki; umaskini; rushwa; na imani za kishirikina.




**Matukio ya ubakaji, ulawiti na unajisi yaliyoripotiwa polisi katika kipindi cha mwezi Januari hadi Juni 2018 & 2019**
Chanzo: Takwimu za Polisi




**Matukio ya ubakaji na ulawiti wa watoto yaliyoripotiwa katika kipindi cha Januari hadi Juni 2017, 2018 na 2019**
Chanzo: Takwimu za polisi, 2017 - 2019

**Mahakama ya Rufaa nchini Tanzania kuamua kwamba ndoa za utotoni zinatakiwa kuondolewa kwenye Sheria ya Ndoa**
Katika hukumu iliyotolewa mwezi Oktoba mwaka 2019, Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ilikubaliana na maamuzi ya Mahakama Kuu ya mwaka 2016, kwamba vifungu vinavyoruhusu ndoa za utotoni kwenye Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 vinakiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kuamuru sheria hiyo ifanyiwe marekebisho kuongeza umri wa kuoa na kuolewa hadi kufikia miaka 18.

**Tatizo kubwa la mimba za utotoni**
Mimba za utotoni ziliendelea kuwa changamoto kubwa mwaka 2019, ambapo matukio mengi zaidi ya mimba hizo yaliripotiwa katika sehemu mbalimbali za Tanzania Bara. Katika kipindi hiki, LHRC ilikusanya jumla ya matukio 836 ya mimba za utotoni yaliyoripotiwa kutoka sehemu mbalimbali za nchi. Kwa kipindi cha kuanzia Januari 2018 hadi Disemba 2019, LHRC ilikusanya matukio zaidi ya 2,543 ya mimba za utotoni, lakini inaamini kuna matukio mengi zaidi ambayo hayajaripotiwa. Wakati huohuo, watoto wanaopata mimba wakiwa shuleni wameendelea kufukuzwa, hivyo kuwa mwisho wa safari ya elimu kwa wengi wao.

**Watoto kuwa katika hatari zaidi ya kuambukizwa Virusi vya UKIMWI (VVU)**
Kuongezeka kwa mimba za utotoni ni ushahidi kwamba watoto wengi wanashiriki katika ngono isiyo salama, hivyo kuwa katika hatari zaidi ya kuambukizwa VVU. Pia, ukatili wa kingono, ikiwemo ubakaji na ulawiti, unawaweka katika hatari ya kuambukizwa VVU. Hii itaathiri juhudi za Tanzania za malengo ya 90-90-90 ya kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu.

**Tatizo la ajira kwa watoto katika maeneo ya migodi mkoani Shinyanga**
Mwaka 2019, tatizo la ajira kwa watoto liliibuka tena upande wa Kanda ya Ziwa, hasa kwenye maeneo ya migodi mkoani Shinyanga. Iliripotiwa kwamba kumekuwa na tabia ya watoto kuacha au kutoroka shule ili kwenda 'kutengeneza pesa' katika migodi, wengine hata kufikia hatua ya kufeli kwa makusudi. Tabia hii pia imechangia kwa kiasi kikubwa utoro mashuleni.

## 5.3. Haki za Watu wenye Ulemavu
Kuna mkataba maalum wa kimataifa unaolinda haki za watu wenye ulemavu, uitwao Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu (CRPD). Haki hizo ni pamoja na haki ya usawa na kutobaguliwa, haki ya kuishi, haki ya usawa mbele ya sheria, haki ya kuwa huru na usalama wa mtu, haki ya kutoteswa, haki dhidi ya ukatili, haki ya elimu, haki ya afya na haki ya kufanya kazi na kuajiriwa. Mkataba huu umeridhiwa na Tanzania na kutungiwa Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2010. Watu wenye ulemavu wanahitaji huduma maalum zitakazowawezesha kufurahia haki za binadamu sawa na watu wengine.

- o Ubaguzi dhidi ya watoto wenye ulemavu uliendelea kuwa changamoto katika ufurahiaji wa haki za watoto hao, hasa maeneo ya vijijini. Katika maeneo haya, kumekuwa na tabia ya wazazi kuwafungia watoto nyumbani, hali inayopelekea kuwanyima haki zao za msingi kama zilivyoanishwa kwenye Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, ikiwemo haki ya kupata elimu.
- o Haki ya elimu kwa watoto wenye ulemavu (elimu jumuishi) pia inakabiliwa na changamoto ya uwepo wa walimu wachache sana ambao wana mafunzo ya elimu maalum. Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti kuhusu elimu ya msingi iliyotolewa na Shirika la Twaweza, ni asilimia 13 tu ya walimu ambao waliohoji wa walikiri kupata mafunzo ya aina yoyote kuhusu elimu maalum.
- o Pia, kuna changamoto ya upungufu wa shule maalum kwa ajili ya watoto wenye ulemavu na changamoto ya kutokuwepo mazingira rafiki kwa watoto hao katika shule nyingi. Kutokuwepo kwa miundombinu rafiki kunachangia tatizo la utoro miongoni mwa watoto wenye ulemavu.
- o Watu wenye ulemavu, hasa wale ambao wana ulemavu wa akili, wapo kwenye hatari zaidi ya kufanyiwa ukatili, ikiwemo ukatili wa kingono.
- o Mashambulizi na mauaji yanayotokana na imani za kishirikina yaliendelea kuleta changamoto kubwa kwa watu wenye ualbino mwaka 2019, na kuwafa nya waishi kwa hofu.
- o Mwaka 2019, Kamati ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Watu wenye Ulemavu ilitoa maamuzi yake kuhusu kesi inayomhusu mwanamke mwenye ualbino kutoka Tanzania, ambaye alishambuliwa kwa mapanga na wanaume wawili alipokuwa nyumbani kwake mwaka 2008, ambapo walimkata mkono mmoja na kuondoka nao na kusababishwa akatwe mkono mwingine hospit ali. Katika maamuzi yake, Kamati ilibaini kwamba Tanzania ilishindwa kute keleza majukumu yak echini ya bara za 5, 15(1), 16 na 17, pamoja na Ibara za 6 na 8 zikisomwa pamoja na Ibara za 5, 15(1), 16 na 17 za Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa mwaka 2006 ya kumlinda mwanamke huyo. Kamati ilamuru mlalamikaji huyo kupatia nafuu madhubuti ya kisheria, ikiwemo fidia, vifaa tiba, na msaada wa kumuwezesha kuendesha maisha yake na kujitegemea kama zamani.

## 5.4. Haki za Wazee

Tofauti na makundi mengine, hakuna mkataba maalum wa kulinda na kusimamia haki za wazee. Hata hivyo, kama binadamu wengine, wazee wana haki mbambali za binadamu kama zilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa. Mikataba hiyo ni pamoja na Mkataba wa Nyongeza kwenye Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Haki za Wanawake barani Afrika (Mkataba wa Maputo); Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiraia na Kisiasa (ICCPR); Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni (ICESCR); na Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu (CRPD).

**Ukatili dhidi ya wazee**

Japokuwa matukio ya ukatili dhidi ya wazee yamepungua kiasi miaka ya hivi karibuni, bado kundi hili maalum linaendelea kukabiliana na changamoto za ukatili wa kimwili na kingono, vitendo ambavyo pia kwa mwaka 2019 vimehusishwa na imani za kishirikina. Katika tukio moja, bibi wa miaka 77, Jema Macheho, aliripotiwa kubakwa hadi kufariki.

**Upatikanaji wa huduma za kijamii**

Changamoto nyingine ambayo imekuwa ikiripotiwa na wazee kwa muda mrefu imekuwa ni kutowza kuzifika huduma za kijamii, hasa huduma ya afya, kwa urahisi. Kwa mwaka 2019 changamoto hii iliripotiwa na wazee Wilaya ya Shinyanga Vijijini mkoani Shinyanga, ambapo walilamika kuhusu upungufu wa dawa wazohitaji katika vituo vya afya.

## 5.5. Haki za Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI

Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wana haki na wajibu mbalimbali kama inavyoainishwa kwenye Sheria ya UKIMWI ya mwaka 2008, ikiwemo haki ya kutobaguliwa, haki ya kupata huduma za afya na wajibu wa kutoambukiza wengine virusi vya UKIMWI kwa makusudi. Sheria ya UKIMWI inakataza ubaguzi dhidi ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na hili ni kosa la jinai ambalo adhabu yake ni faini isiyopungua Shilingi Milioni 2 au kifungo kisichozidi mwaka 1 au vyote.

Changamoto kubwa kwa upande wa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI imeendelea kuwa ubaguzi na unyanyapaa. Ubaguzi na unyanyapaa huo umewafanya washindwe kufurahia haki zao kwa amani na kuwafanya wengine kuona aibu au kujisikia vibaya hata kufikia huduma za afya. Wanaweka na wasichana wanaathirika zaidi ya ubaguzi na unyanyapaa, ikiwemo ndani ya familia, shuleni na mahala pa kazi.

# SURA YA SITA: MIFUMO YA ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU

**Utangulizi**

Mifumo ya ulinzi wa haki za binadamu inajumuisha sheria zinazolinda haki za binadamu na taasisi mbalimbali ambazo zina jukumu la kusimamia sheria hizo na kulinda na kuimarisha haki za binadamu. Kuna mifumo ya kitaifa, mifumo ya kikanda na mifumo ya kimataifa.

## 6.1. Mifumo ya Kitaifa ya Ulinzi wa Haki za Binadamu

Mifumo ya kitaifa ya ulinzi wa haki za binadamu inajumuisha taasisi muhimu kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG), Mahakama na Vyombo vya Dola kama vile Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza. Vyombo hivi vipo kwa mujibu wa sheria.

**Wajibu wa mifumo ya kitaifa ya ulinzi wa haki za binadamu**

**Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora:** Tume hii ilianzishwa chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na jukumu lake kubwa ni kukuza, kuimarisha na kulinda haki za binadamu, ikihakikisha zinaheshimiwa, pamoja na kusimamia utawala bora. Pia, Tume huishauri Serikali na taasisi zake kwenye masuala ya haki za binadamu na utawala bora na hupokea malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu toka kwa wananchi na kuyafanyia kazi.

**Mahakama:** Mahakama ni chombo muhimu sana katika ulinzi wa haki za binadamu, ambacho hutoa tafsiri mbalimbali za sheria zinazohusu haki za binadamu, husikiliza kesi na kutoa maamuzi na nafuu za kisheria. Mhimili huu ni muhimu na hutakiwa kuwa huru katika kuchunga mienendo na matendo ya mihimili mingine, ambayo ni Serikali na Bunge. Mhimili huu una jukumu la kusimamia utekelezaji wa haki za binadamu na kuhakikisha kwamba pale ambapo umetokea ukiukwaji wa haki hizo, basi nafuu madhubuti na stahiki za kisheria zinatolewa.
Vyombo vya dola: Hivi ni pamoja na Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza, ambavyo vina nafasi na jukumu kubwa la kulinda na kuimarisha haki za binadamu. Jeshi la Polisi lina jukumu la kusaidia watu kufikia haki kwa kufanya uchunguzi na kuwafikisha watuhumiwa au wavunjifu wa haki za binadamu mahakamani. Magereza huwalinda wanajamii dhidi ya watu waliohukumiwa kutumikia vifungo kwa kufanya uhalifu ambao unahatarisha haki za binadamu, na hivyo uwepo wake huimarisha ulinzi wa haki za binadamu.

**Hatua zilizochukuliwa na mifumo ya kitaifa ya ulinzi wa haki za binadamu kukuza na kulinda haki za binadamu.**

Jeshi la Polisi liliendelea kuchukua hatua mbalimbali kuwalinda wananchi na mali zao, ikiwemo kuwakamata watuhumiwa wa ukiukwaji wa haki za binadamu, wakiwemo watuhumiwa wa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto na wanawake. Madawati ya jinsia na watoto ya polisi pia yaliendelea kukusanya na kushughulikia matukio ya ukatili dhidi wanawake na watoto.


Mhimili wa Mahakama uliendelea kuchukua hatua mbalimbali kuboresha upatikanaji wa haki, ikiwemo: ujenzi wa majengo ya mahakama na ukarabati wa majengo ya zamani; matumizi ya TEHAMA katika kuongeza kasi ya usikilizaji mashauri na kupunguza gharama za kuhudhuria mahakamani; uanzishwaji wa mahakama za kutembea; kufanya ukaguzi wa mahakama; uanzishwaji wa vituo jumuishi vya huduma za kimahakama; kupungza mrundikano wa kesi; na kutengeneza mwongozo wa utoaji adhabu.

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora nayo iliendelea na utekelezaji wa shughuli zake kama taasisi ya kitaifa ya haki za binadamu, ikiwemo: kueneza uelewa kuhusu haki na wajibu wa binadamu; kupokea malalamiko kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu na kuyafanyia kazi; kufanya uchunguzi kuhusu masuala ya ukiukwaji wa haki za binadamu na kanuni za utawala bora; kufanya tafiti na kutoa elimu kuhusu haki za binadamu na utawala bora; kufanya uchunguzi kuhusu mienendo ya watu au taasisi kuhusiana na utendaji wa kazi zao au matumizi mabaya ya mamlaka yao; na kuzishauri Serikali, taasisi za serikali na sekta binafsi kuhusu masuala ya haki za binadamu na utawala bora.

Mwaka 2019 pia ulikuwa mwaka mzuri kwa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ambapo hatimaye ilipata Mwenyekiti mpya na makamishna wapya wa haki za binadamu. Mnano mwezi Septemba mwaka 2019, Mh. Rais John Magufuli alimteua Jaji Mstaafu Mathew Mwaimu kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Mohamed Khamis Hamis, kutoka Idara ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai Zanzibar, alichaguliwa kuwa Kaimu Mwenyekiti wa Tume. Pia, Makamishna watano wa Tume walichaguliwa, ambao ni: Dkt. Fatma Rashid Khalfani (Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Zanzibar); Dkt. Thomas Masanja (Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino); Bi. Amina Talib Ali (Afisa Mwandamizi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar); Bw. Khatib Mwinyi Chande (Mhadhiri wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania); na Bw. Nyanda Josiah Shuli (Afisa Mwandamizi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango).

Kwa upande wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), nayo ilendelea kutekeleza majukumu yake ya kuzuia na kupambana na rushwa katika maeneo mbalimbali ya nchi, ikiwemo kueneza uelewa kuhusu rushwa na madhara yake pamoja na kupeleleza kesi za rushwa na kuwafikisha watuhumiwa mahakamani. Utafiti kuhusu hali ya rushwa duniani uliofanywa na Shirika la Transparency International mwaka 2019 unaonyesha kuongezeka kwa juhudi za kupambana na rushwa, japokuwa tatizo la rushwa bado ni kubwa nchini Tanzania.

Ripoti ya shirika hilo ya mwaka 2017 ilionyesha kwamba Tanzania ilipata pointi 36 kati ya 100 (kadri pointi zinavyopanda maana yake rushwa inapungua) mwaka huo, ikipanda kwa nafasi 13 ukilinganisha na mwaka 2016. Kwa mwaka 2018, Tanzania ilipata tena pointi 36 kati ya 100 na kupanda kwa nafasi 4 zaidi hadi kufikia nafasi ya 99. Kwa mwaka 2019, Tanzania ilipanda tena kwa nafasi 3 hadi nafasi ya 96 kati ya nchi 180, ikipata pointi 37 kati ya 100.




**Alama ilizopata Tanzania katika Utafiti kuhusu Mitazamo ya Rushwa kuanzia mwaka 2014 hadi 2019**

Chanzo: Ripoti za Mitazamo kuhusu Rushwa ya shirika la Transparency International za miaka ya 2014 hadi 2019

**Changamoto zinazoikabili mifumo ya kitaifa ya ulinzi wa haki za binadamu**
Changamoto zinazoikbaili mifumo ya kitaifa ya ulinzi wa haki za binadamu nchini Tanzania ni pamoja na: rushwa; ucheleweshaji katika uchunguzi/upelelezi na uendeshaji wa kesi; mazingira duni ya kufanyia kazi kutokana na uhaba wa vifaa vya kazi; upungufu wa maafisa wa vyombo vya dola na watumishi wa mahakama; mrundikano wa wafungwa na mahabusu magerezani; ufinyu wa bajet; upungufu wa majengo na vifaa; uelewa mdogo kuhusu haki za binadamu na umuhimu wa kufuata utaratibu wa haki jinai; na vitendo vya rushwa na vitendo vingine vilivyo kinyume na maadili miongoni mwa maafisa wa Jeshi la Polisi.

## 6.2. Mifumo ya Kikanda na Kimataifa ya Ulinzi wa Haki za Binadamu
Mifumo ya kikanda na kimataifa ya ulinzi wa haki za binadamu inajumuisha mikataba mbalimbali ya haki za binadamu, ambayo inaunda vyombo mbalimbali vya kusimamia utekelezaji wa mikataba hiyo na nchi wanachama.

Chini ya Umoja wa Mataifa kuna mfumo wa kutathmini haki za binadamu uitwao Mpango wa Kimataifa wa Kujitathmini juu ya Masuala ya Haki za Binadamu (UPR) au Tathmini ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa, ambao unasimamiwa na Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa. Mfumo huu unalenga kuboresha hali ya haki za binadamu katika nchi 193 wanachama wa Umoja wa Mataifa. Nchi wanachama, ikiwemo Tanzania, huwasilisha ripoti kila baada ya miaka 5 ikielezea ni hatua gani imechukua kuboresha haki za binadamu kulingana na wajibu ulioanishwa katika mikataba mbalimbali ya haki za binadamu ambayo zimeridhia. Mara ya mwisho Tanzania kushiriki katika mchakato huu ni mwaka 2016, ambapo Serikali ilipeleka ripoti yake ya utekelezaji wa haki za binadamu na mashirika yasiyo ya kiserikali kupeleka ripoti kivuli.

Ukiacha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, vyombo vingine katika ngazi za kikanda na kimataifa zinazosimamia utekelezaji wa majukumu yanayohusiana na haki za binadamu katika mikataba iliyoridhiwa ni pamoja na Kamati ya Haki za Binadamu ya Umoja wa Mataifa (HRC), Kamati ya Haki za Mtoto (CRC), Kamati ya Haki za Kiuchumi, Kijamii  na Kiutamaduni (CESCR), Kamati ya Kuondoa aina Zozote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW), Kamati ya Haki za Watu wenye Ulemavu (CRPD) na Kamati ya Wataalamu katika Masuala ya Haki na Ustawi wa Mtoto Afrika (ACERWC). Tanzania ina wajibu wa kutoa taarifa za haki za binadamu kwa vyombo hivi kila baada ya muda fulani. Hata hivyo, siyo mara zote ripoti hizo zimekuwa zikitumwa au kutumwa kwa wakati.

Pia, kwa upande wa Afrika kuna Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ambayo ipo Arusha – Tanzania) na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ambapo nchi wanachama wa Umoja wa Afrika hutakiwa kutuma ripoti na pia hupokea na kusikiliza malalamiko kuhusu haki za binadamu).  Kuna taratibu za kupekeleka malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu endapo mhanga wa ukiuwaji huo hajaridhika na nafuu aliyopata katika mifumo ya kitaifa ya utoaji haki.

Ugumu wa utekelezaji wa maamuzi na hukumu zinazotolewa na mifumo ya kikanda na kimataifa ya ulinzi wa haki za binadamu

Pamoja na mifumo ya kikanda na kimataifa kutoa hukumu mbalimbali zinazoihusisha nchi ya Tanzania, utekelezaji wa maamuzi na hukumu hizo umeendelea kuwa changamoto, has kwa kuwa utekelezaji wake hutegemea zaidi utashi wa kisiasa. Hili limekuwa tatizo kubwa barani Afrika, ikiwemo nchini Tanzania.

Uwasilishaji wa ripoti za Tanzania kuhusu utekelezaji wa haki za binadamu kwa mifumo ya kikanda na kimataifa ya haki za binadamu

Kama ilivyoelezwa hapo juu, Tanzania ina wajibu chini ya mikataba mbalimbali iliyoridhia wa kuwasilisha ripoti kuhusu utekelezaji wa haki za binadamu nchini kwa mifumo mbalimbali ya kikanda na kimataifa. Mwaka 2019, Waziri wa Katiba na Sheria, Mh. Balozi Dkt. Augustine Mahiga (MB), alielezea kwamba Tanzania inaandaa ripoti yake kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa mwaka 2006.

**Tanzania kujitoa katika tamko linalowezesha wananchi na mashirika yasiyo ya kiserikali kupeleka kesi katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Watu na Binadamu**

Mwaka 2019 Tanzania ilikuwa nchi ya pili barani Afrika kujiondoa katika tamko linalowezesha wananchi na mashirika yasiyo ya kiserikali kupeleka kesi katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Watu na Binadamu, baada ya Rwanda kufanya hivyo mwaka 2016.

# SURA YA SABA: HITIMISHO NA MAPENDEKEZO MUHIMU

**Hitimisho**

**Haki za Kiraia na Kisiasa:** Hali ya haki za kiraia na kisiasa ilidorora kiasi mwaka 2019 ukilinganisha na mwaka 2018. Sababu kubwa za kudorora kwa haki hizi ni ukiukwaji wa haki ya kuishi, haki ya kuwa huru na salama, haki ya usawa mbele ya sheria na haki za ushiriki (uhuru wa kujieleza, uhuru wa kujumuika na uhuru wa kukusanyika). Kwa upande wa haki ya kuishi, mambo makuu yaliyochangia ukikuwaji wa haki hiyo ni adhabu ya kifo, mauaji ya watoto, mauaji ya wanawake, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, ajali za barabarani na mauaji yanayotokana na kujichukulia sheria mkononi. Kwa upande wa haki ya kuwa huru na salama, haki ya usawa mbele ya sheria na haki za ushiriki, ukiukwaji wa haki hizi ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na uwepo na utekelezaji wa sheria zinazominya haki hizo, marekebisho ya sheria ambayo yanaminya haki kinyume na sheria na viwango vya kikanda na kimataifa, uahirishaji wa mara kwa mara wa kesi, kutozingatia kanuni ya kutotendewa kama mtu mwenye hatia mpaka mahakama itakavyothibitisha vinginevyo, na ukamataji na uwekaji kuzuizini wa watu kinyume na sheria.

**Haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni:** Kwa mwaka 2019, kwa ujumla hali ya haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni haikubadilika ukilinganisha na mwaka 2018, isipokuwa kwa haki ya upatikanaji elimu, ambayo iliendelea kuimarishwa kupitia utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo. Utekelezaji Madhubuti wa haki za muhimu kama haki ya elimu, haki ya afya na haki ya maji safi na salama uliendelea kuathiriwa na upungufu wa bajeti katika sekta za afya, elimu na maji, fedha za bajeti kutofika zote kama zilivyopangwa na ucheleweshaji katika kutuma fedha za bajeti wa wizara na idara husika. Changamoto nyingine iliyoendelea kuzikabili sekta hizi muhimu ni upungufu wa wataalamu na wafanyakazi wengine, wakati kwa upande wa elimu kulikuwa pia na changamoto ya mazingira ya kujifunza katika shule za msingi na sekondari, ambayo yaliendelea kuathiriwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo upungufu wa matundu ya vyoo na wanafunzi kulazimika kutembea umbali mrefu kufika shuleni. Changamoto zaidi zilizoathiri ufurahiaji na utekelezaji wa haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni ni pamoja na malimbikizo ya madai ya walimu na ukiukwaji wa haki za wafanyakazi katika makampuni binafsi.

**Haki za kiujumla:** Ufurahiaji na utekelezaji wa haki ya maendeleo uliimarika kiasi mwaka 2019, ukichangiwa kwa kiasi kikubwa na maendeleo ya miundombinu, ambayo ni maendeleo ya kiuchumi. Hata hivyo, changamoto kubwa ilindelea kuwa kwenye mandeleo ya kibinadamu, maendeleo ya kisiasa na maendeleo ya kijamii. Changamoto zinazoathiri utekelezaji madhubuti wa haki za kiujumla ni pamoja na usimamizi mbovu wa rasilimali asilia, ukwepaji kodi, misamaha ya kodi, na mianya katika sheria za madini na maliasili.

**Haki za makundi maalum:** Hali ya haki za makundi maalum, hasa wanawake na watoto, ilidorora zaidi mwaka 2019. Hali hii ilichangiwa ziadi na kuongezeka kwa matukio ya ukatili wa kingono na kimwili dhidi ya wanawake na watoto. Vitendo vya ukatili wa kimwini vilipelekea majeraha makubwa kwenye miili ya wahanga na vingine kupelekea vifo vyao, huku vitendo vya ukatili wa kingono, hasa ubakaji na ulawiti, vikishamiri. Watoto waliendelea kuwa wahanga wakuu wa vitendo vya ubakaji na ulawiti. Kwa upande wa watu wenye ulemavu, hali ya haki zao iliimarika kiasi, hali iliyochangiwa na kupungua kwa matukio ya ukiukwaji wa haki zao. Hata hivyo, watu wenye ulemavu wa Ngozi waliendelea kuishi kwa wasiwasi kutokana na mashambulizi dhidi yao, japokuwa mashambulizi hayo yamepungua kwa kiasi kikubwa katika miaka ya hivi karibuni. Wasiwasi huu kwa upande wa watu wenye ulemavu umeongezeka kipindi hiki kwa sababu ni kipindi cha uchaguzi, ambapo kwa kipindi cha nyuma ilionekana kwamba mashambulizi dhidi ya watu wenye ualbino yalikuwa yanaongezeka kipindi cha uchaguzi. Haki za wazee ziliimarika mwaka 2019, hii ikichangiwa kwa kiasi kikubwa kupungua kwa matukio ya ukatili dhidi yao; na kwa upande wa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI changamoto kubwa iliendelea kuwa ubaguzi na unyanyapaa wanaofanyiwa.

## Mapendekezo Muhimu

### 1. HAKI ZA KIRAIA NA KISIASA

**Serikali**

- Kwa kuwa Tanzania ni mojawapo ya nchi ambazo hazitekelezi adhabu ya kifo, Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, itangaze rasmi kwamba imesitisha adhabu ya kifo na kufanya marekebisho ya sheria kuondoa adhabu hiyo kwenye sheria.
- Wizara ya Katiba na Sheria ianzishe mchakato wa kufanyia marekebisho sheria zote zinazominya uhuru wa kujieleza, uhuru wa kujumuika na uhuru wa kuku sanyika, ikiwemo Kanuni za Maudhui ya Mtandao za mwaka 2018 na Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992.

- Serikali kufanyia marekebisho Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 kulin gana na maamuzi ya Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki.
- Jeshi la Polisi kuongeza kasi ya upelelezi wa kesi ili kulinda na kuimarisha haki ya kuwa huru na salama na haki ya usawa mbele ya sheria.
- Maafisa polisi kutumia vizuri mamlaka yao chini ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi ili kulinda uhuru wa kukusanyika, wakihakikisha hawaingilii uhuru wa kukusanyika au kukataza mikusanyiko kinyume na sheria.
- Maafisa wa serikali na wanachama wa vyama vya siasa kuzingatia uvumilivu wa kisiasa ili kulinda amani na utulivu.
- Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria, kutengeneza chombo huru cha kusi mamia na kukuza uwajibikaji ndani ya vyombo vya dola.
- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba maafisa wa polisi katika ngazi zote wanapata mafunzo ya mara kwa mara kuhusu Kanuni za Msingi za Umoja wa Mataifa za Matumizi ya Nguvu na Silaha za Moto kwa Maafisa wa Vyombo vya Dola, pamoja na mafunzo kuhusu haki za binadamu kwa ujumla, kama sehemu ya kuongeza uwajibikaji na kupun guza mauaji yanayosababishwa na matumizi ya nguvu kupita kiasi ya maafisa wa vyombo vya dola.
- Jeshi la Polisi lihakikishe maafisa wa polisi kuepuka ukamataji na uwekaji kuzuiz ini wa watuhumiwa kinyume na sheria na kuhakikisha watuhumiwa wanapele kwa mbelel ya mahakama katika muda usiozidi masaa 24 kama inavyotakiwa kisheria ili kulinda haki ya kuwa huru na salama na haki ya usawa mbele ya sheria.
- Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba maafisa wa polisi kuepuka kujihusisha na vitendo vya ubambikaji wa kesi na vitendo vingine kinyume na maadili ya Jeshi la Polisi.
- Serikali kuridhia na kutungia sheria Mkataba dhidi ya Mateso na Adhabu au Vitendo vingine vya Kikatili, visivyo vya Kibinadamu, vya Kinyama na vyenye Kud halilisha wa Mwaka 1984 (Mkataba dhidi ya Uteswaji) ili kuongeza ulinzi wa haki ya kutoteswa.

**Wadau wengine**

- Asasi za kiraia ziongeze juhudi za kueneza uelewa wa umma kuhusu taratibu za kisheria na haki za kiraia na kisiasa, pamoja na kuwahamasisha wanajamii kutii sheria na kuheshimu haki za binadamu ili kulinda haki hizo, ikiwemo haki ya kuishi. Kwa mfano, kwa upande wa mashambulizi dhidi ya mtuhumiwa wa uhali fu yanayofanywa na 'watu wenye hasira kali' kuna haja ya kutoa elimu kuhusu makosa yenye dhamana.
- Asasi za kiraia na mashirika ya kidini kutumia nafasi zao kukemea na kueneza uelewa kuhusu wananchi kujichukulia sheria mkononi, adhabu ya kifo, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, mashambulizi dhidi ya watu wenye ulemavu wa Ngozi na ajali za barabarani pamoja na madhara yake kwenye haki za binadamu.

- o Asasi za kiraia zishirikiane kwa karibu na Tume ya Haki za Binadamu kutoa ma funzo ya mara kwa mara kuhusu haki za binadamu kwa majaji, mahakimu na wanataaluma wengine wa sheria ili kuwaongezea uelewa kuhusu haki za binadamu na nafasi yao katika kuzikuza na kuzilinda, ikiwemo haki ya usawa mbele ya sheria, pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa haki.

**Wanajamii**

- o Wanajamii kuepuka kujichukulia sheria mkononi na kutafuta nafuu za kisheria katika ngazi ya juu zaidi ya mfumo wa haki pale ambapo hawajafurahishwa na hukumu ya kesi.
- o Viongozi wa kidini na wa kijadi kutumia nafasi zao kukemea matukio ya ukiuk waji wa haki za kiraia, hasa haki ya kuishi, uhuru wa kujieleza na haki ya kuto teswa, kama sehemu ya kukuza haki hizi.
- o Wanajamii kutoa taarifa na kufichua matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu kwa mamlaka husika ili kulinda haki hizo na kuhakikisha watuhumiwa wana fikishwa mbele ya vyombo vya sheria.

## 2. HAKI ZA KIUCHUMI, KIJAMII NA KIUTAMADUNI

**Serikali**

- o Serikali, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, kuongeza bajeti kwenye sekta muhimu za afya, elimu na maji ili kuongeza upatikanaji wa huduma bora za afya, elimu, na maji, kulingana na viwango vya kimataifa kuhusiana na bajeti za sekta hizi, sambamba na kuhakikisha fedha zilizotengwa zinawasilishwa zote na kwa wakati.
- o Serikali, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, kuongeza bajeti katika sekta ya kilimo, ambayo ndiyo mwajiri mkuu, ili kukuza haki ya maendeleo na haki ha kufanya kazi; na kuongeza uwekezaji katika umwagiliaji ili kuimarisha haki ya chakula.
- o Serikali, kupitia Wizara ya Elimu na Ufundi, kutatua changamoto mbalimbali zin azoikumba sekta ya elimu, kama vile mazingira duni ya walimu kufanyia kazi na upungufu wa madarasa na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Wizara ihakikishe nyumba za walimu zinajengwa na walimu wanalipwa malimbikizo yao. Hatua hizi ni Muhimu katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, hususan lengo la 4, na malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.
- o Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuweka mikakati ya kuzuia ukatili dhidi ya watoto unaofanywa na walimu wa kiume shuleni.
- o Serikali kuhakikisha kwamba taasisi zake zinalipa bili za maji zinazodaiwa kwa wakati ili kuziwezesha mamlaka zinazosimamia rasilimali ya maji kutekeleza kazi zake ipasavyo.

- Wizara ya Maji kuongeza juhudi za kudhibiti na kutatua tatizo la upotevu wa maji, wambao umekuwa ukisababisha hasara ya mabilioni ya fedha.
- Kuhusiana na wasichana wanaopata mimba wakiwa shuleni, LHRC inaendelea kuisihi Serikali kufikiria upya na kubadilisha msimamo wake wa wanafunzi hao kutoruhusiwa kuendelea na masomo, ili kulinda haki ya elimu kwa wasichana kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.
- Wizara ya Elimu na Ufundi iongeze upatikanaji wa elimu kwa watoto wenye ulemavu (elimu jumuishi) kwa kuhakikisha uwepo wa miundombinu inayohitaji ka, walimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

**Wadau wengine**

- Asasi za kiraia kushirikiana na wizara husika, kama vile wizara inayohusika na masuala ya jinsia na wizara inayohusika na ardhi, katika kukuza na kulinda haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, ikiwemo kufanya kampeni za pamoja na kueneza uelewa kuhusu haki hizo.
- Asasi za kiraia kushirikiana na Wizara ya Kazi na Sheria kueneza uelewa kuhusu sheria za kazi, haki na wajibu.
- Sekta binafsi ishirikiane na Serikali kuwekeza katika miradi ya maji ili kuongeza upatikanaji wa huduma za maji. Hili linaweza kufanyika kama sehemu ya uwaji bikaji wa makampuni kijamii.

**Wanajamii**

- Umma ujenge tabia ya kutafuta maarifa na taarifa mbalimbali kuhusu haki zao za kiuchumi, ikiwemo haki ya kufanya kazi na haki ya kumiliki mali, ikiwemo kupitia matoleo ya lugha nyepesi ya sheria kuhusu haki hizo yanayotolewa na taasisi na mashirika mbalimbali.
- Wanajamii kutoa taarifa kuhusu matukio ya ukikuwaji wa haki za kiuchumi kwa mamlaka husika, ikiwemo vyama vya wafanyakazi na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.
- Wazazi kufanya juhudi za kuelewa majukumu yao kuhusiana na watoto chini ya Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 na kufanya juhudi za kuhakikisha kwamba watoto wao wanafurahia na kutekeleza haki zao, ikiwemo haki ya kupata elimu na uhuru dhidi ya ukatili.
- Wanajamii kuilinda miundombinu mbalimbali na kujiepusha na tabia ya kuihari bu, hasa miundombinu ya maji. Pia, wana jukumu la kutoa taarifa kwa mamlaka husika kuhusu matukio ya uharibifu wa miundombinu.
- Pale inapowezekana, wanajamii kujikusanya na kuisaida Serikali kushughulikia baadhi ya changamoto katika sekta ya elimu, kama vile upungufu wa madawati na upungufu wa matundu vya vyoo.

## 3. HAKI ZA KIUJUMLA

**Serikali**

- o Serikali, kupitia TAKUKURU, kuongeza juhudi za kupambana na rushwa katika sekta ya madini, ambayo inaathiri ufurahiaji wa haki ya maendeleo na haki ya kufurahia na kufaidika na maliasili.
- o Wizara ya Utalii na Maliasili kuhakikisha utekelezaji Madhubuti wa sheria za mali asili.
- o Serikali, kupitia Kituo cha Uwezekaji Tanzania, kuhakikisha wawekezaji wana heshimu haki za binadamu na kufuata sheria za nchi katika utekelzaji wa shu ghuli zao.
- o Serikali kuongeza juhudi za kupambana na ukwepaji kodi, hasa katika sekta ya madini na kuhakisha makampuni yanayokwepa kodi yanawajibishwa kisheria.

**Wadau wengine**

- o Asasi za kiraia na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kueneza uelewa kuhusu haki ya maendeleo na haki ya kufurahia na kufaidika na maliasili.
- o Asasi za kiraia kutambua mianya katika utekelezaji wa haki ya kufurahia na kufaidika na maliasili na kuishauri Serikali ipasavyo.

**Wanajamii**

- o Wanajamii wanahamasishwa kutunza na kulinda maliasili, kwani ni wajibu wao kikatiba.
- o Wanajamii pia wanahamasishwa kutoa taarifa kuhusu matukio yanayohatarisha haki za kiuchumi, ikiwemo ujangili.

## 4. HAKI ZA MAKUNDI MAALUM

**Serikali**

- o Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupeleka bungeni muswada wa kutunga sheria maalum dhidi ya ukatili wa kijinsia.
- o Serikali, kupitia Wizara ya Katiba na Sheria na Tume ya Kurekebisha Sheria, kufa nya mapitio na kuondoa au kurekebisha sheria zote zinazowabagua wanawake na kuwanyima haki zao kinyume na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa iliyoridhiwa na Tanzania.
- o Serikali, kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, kuingiza elimu ya jinsia katika mitaala ya elimu katika ngazi zote za elimu.
- o Serikali kutimiza wajibu wake chini ya mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa kuhusu haki za watoto na kulingana na hukumu ya Mahakama ya Rufaa kwenye kesi ya Rebeca Gyumi ya mwaka 2019 kufanya mabadiliko ya sheria ili kuondoa ndoa za utotoni kwenye Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971.
- o Jeshi la Polisi na Mhimili wa Mahakama kuongeza kasi ya uchunguzi na uende shaji wa kesi za ukatili dhidi ya watoto.

**Wadau wengine**

- Asasi za kiraia na vitengo vya ustawi wa jamii kuongeza juhudi za kueneza uelewa kuhusu ukatili dhidi ya wanawake na watoto na kuhamasisha wanajamii kutoa taarifa kuhusu matukio ya namna hiyo kwa mamlaka husika ili watuhumi wa wakamatwe na kufikishwa mbele ya vyombo vya sheria.
- Asasi za kiraia zishirikiane na Serikali kuhakikisha utekelezaji madhubuti wa Mkataba wa Haki za Mtoto ili kulinda haki za watoto wote, ikiwemo watoto wana oishi mtaani na watoto wenye ulemavu.

- Asasi za kiraia ziendelee kueneza uelewa kuhusu haki za wazee na kufanya kampeni za kupinga na kutokomeza ukatili na ubaguzi dhidi ya wazee.
- Wadau mbalmbali kuimarisha mifumo ya utoaji taarifa ili kuwawezesha wana wake, hasa wanaokaa kijijini, ili kuwawezesha kutoa taarifa kirahisi.

**Wanajamii**

- Wanajamii kutekeleza wajibu wao wa kuwalinda wanawake na watoto na kuz ilinda haki zao, pamoja na kujiepusha na vitendo vya unyanyasaji na ukatili dhidi ya wanawake na watoto.
- Wanajamii kujiepusha na vitendo vya ubaguzi dhidi ya watoto, ikiwemo watoto wa mtaani na watoto wenye ulemavu.
- Wanajamii kujiepusha na tabia ya kuwalinda watuhumiwa wa ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa sababu tu ya kutaka 'kuficha aibu ya familia.'
- Wanawake na watoto watoe taarifa kuhusu matukio ya ukatili wanayofanyiwa na kutoa ushirikiano kwa mamlaka husika ili sheria ichukue mkondo wake na wao wapate huduma na msaada wanaohitaji, ikiwemo huduma za kiafya na kisheria. Pia, wanahamasishwa kushirikiana na waendesha mashtaka na maafisa wa ustawi wa jamii katika kutoa ushahidi mahakamani ili kuhakikisha watuhumiwa wa vitendo vya ukatili wanawajibishwa na haki inatendeka.

# MAMBO MAKUU YANAYOATHIRI ULINZI WA HAKI ZA BINADAMU

- Sheria mbaya au zinazominya haki, ambazo zinakinzana na viwango na kanuni za haki za binadamu.
- Uelewa mdogo wa sheria, zikiwemo zinazohusu haki za binadamu, kwa pande zote
- Kutofuata utaratibu wa kisheria
- Ufinyu wa bajeti katika sekta muhimu
- Rushwa na ukweapaji kodi
- Uvivu na imani za kishirikina
- Uelewa mdogo wa haki za binadamu miongoni mwa wananchi na viongozi wao
- Kukosekana uwajibakaji wa kitaasisi na hata wa mtu mmoja mmoja
- Uendelezwaji wa mila potofu na kandamizi mfano-ukeketaji, ndoa na mimba za utotoni
- Kupungua kwa nafasi ya ushiriki wa wananchi.



LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE
LHRC
KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Shiriki kulinda na kudumisha haki za binadamu

## Changia Haki

### Changia kwa Airtel Money

Hatua ya 1: Ingia kwenye Menyu ya Airtel Money (*150*60#)
Hatua ya 2: Chagua (5) Lipia Bili
Hatua ya 3: Chagua (4) Ingiza Namba ya Kampuni
Hatua ya 4: Ingiza Namba ya Kampuni (275454)
Hatua ya 5: Weka Kiasi Unachotaka Kuchangia
Hatua ya 6: Ingiza Namba ya kumbukumbu (1234)
Hatua ya 7: Weka Namba ya Siri Kuthibitisha Muamala

### Changia kwa TigoPesa

Hatua ya 1: Ingia kwenye Menyu ya Tigo Pesa (*150*01#)
Hatua ya 2: Chagua (4) Lipia Bili
Hatua ya 3: Chagua (3) Ingiza Namba ya Kampuni
Hatua ya 4: Ingiza Namba ya Kampuni (275454)
Hatua ya 5: Weka Kumbukumbu Namba (1234)
Hatua ya 6: Weka Kiasi Unachotaka Kuchangia
Hatua ya 7: Ingiza Namba ya Siri Kuthibitisha Muamala

### Changia M-Pesa

Hatua ya 1: Ingia kwenye Menyu ya M-Pesa (*150*00#)
Hatua ya 2: Chagua (4) Lipa kwa Mpesa
Hatua ya 3: Chagua (4) Namba ya Kampuni
Hatua ya 4: Weka Namba ya Kampuni (275454)
Hatua ya 5: Weka Namba ya Kumbukumbu ya Malipo (1234)
Hatua ya 6: Weka Kiasi
Hatua ya 7: Weka Namba ya Siri
Hatua ya 8: Bonyeza 1 Kuthibitisha Muamala

@humanrightstz Haki TV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*

Sweden Sverige

Norwegian Embassy

FORD FOUNDATION

Irish Aid
Rialtas na hÉireann
Government of Ireland

Ministry for Foreign Affairs of Finland


**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU - MAKAO MAKUU**
Jengo la Jaji Lugakingira, Kijitonyama,
S.L.P 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz **Tovuti:** www.humanrights.or.tz

**OFISI YA ARUSHA,**
Mtaa wa Olerian Kitalu Na. 116/5, Sakina kwa Iddi
S.L.P 15243, Arusha, Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**KITUO CHA MSAADA WA SHERIA - KINONDONI**
Mtaa wa Isere – Kinondoni, S.L.P 79633,
Dar es Salaam, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 27612015/6
**Barua pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

**OFISI YA DODOMA**
Kitalu Na. Area D, **S.L.P** 2289, Dodoma, Tanzania
**Phone/Fax:**+255 262350050 **Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV


*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*